Jumamosi Juni 8, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • No. 0581701

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US

**KORTI** Rufani yatengua kaka kuwa msimamizi mirathi ya dada

UKURASA 2




**ALIYEFUNGWA** jela maisha kwa kubaka aachiwa huru

UKURASA 5

**VYAMA** ruksa mawakala daftari la wapigakura

UKURASA 7



**KANYE KAYAKANYAGA TENA**

UKURASA 14

# Mtego ulivyowanasa matapeli eneo NSSF

**WALITAKA** 'kumpiga' bibi mil. 8/- Waziri Silaa apiga 'stop'...*Ukurasa 2*



Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa, akizungumza na waandishi wa habari, baada ya kukamatwa kwa watuhumiwa wanaodaiwa kuwatapeli wananchi na kuwauzia ardhi inayomilikiwa na NSSF katika Mtaa wa Malela, Toangoma, Temeke, Dar es Salaam jana. Picha ndogo: Watuhumiwa hao, wakiwa chini ya ulinzi wa Polisi baada ya kukamatwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



## Nchimbi ataka wabadhirifu, wezi wa fedha waombewe

**Na Romana Mallya,** KOROGWE

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, amewataka Watanzania kuwaombea wenye roho za wizi, ubadhirifu ili ziwatoke.

Amesema haiwezekani Rais Samia Suluhu Hassan anahangaika kutafuta fedha ndani na nje ya nchi usiku na mchana na kuzishusha chini halafu hazitumiki kama ilivyokusudiwa.

Akizungumza jana na wananchi Korogwe, mkoani Tanga...

Endelea Uk. 3

**Wakurugenzi waonywa pesa za uhamisho, likizo walimu**

UKURASA 8

**MICHEZO** AZAM YATHIBITISHA KUMNASA MSHAMBULIAJI MASHUJAA FC UK 23

MAONI, KATUNI UK.6

# Mtego ulivyowanasa matapeli eneo la NSSF

Na Mwandishi Wetu

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa, amempa siku 14 Kamishna wa Ardhi Mkoa wa Dar es Salaam kuwaondoa watu wote waliovamia ardhi inayomilikiwa na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), mtaa wa Malela, Toangoma, Kigamboni mkoani Dar es Salaam.

Silaa alitoa agizo hili juzi katika mtaa wa Malela baada ya kuwakamata watuhumiwa sugu wanne wanaodaiwa kuwatapeli wananchi na kuwauzia ardhi, baada ya NSSF kuweka mtego uliofanikisha kutiwa nguvuni kwa watu hao.

Alisema kutokana na kuenea kwa matukio hayo, anapiga marufuku wenyeviti wa serikali za mitaa kujihusisha na mauzo ya ardhi pamoja na nyaraka za serikali za mitaa kutumika kuuzia viwanja.

Waziri alisema hivi sasa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi inafanya marekebisho ya GN ya mwaka 2021, inayotoa nyaraka zinazotumika katika mauzo ya ardhi na wanatarajia kutoa nyaraka mpya za kuuza maeneo nchini.

"Watu wa serikali za mitaa wakae mbali na shughuli za ardhi. Kwa hili watatusamehe. Niko makini sana na masuala ya ardhi pamoja na utapeli wa ardhi unaoendelea," alisema.

Silaa pia aliagiza Jeshi la Polisi kuwakamata watuhumiwa hao ili wachukuliwe hatua za kisheria huku akimwagiza Mkuu wa Upelelezi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam (ZCO) kufanya operesheni maalumu katika eneo hilo ili kuwakamata watuhumiwa wengine na kuchukuliwa hatua za kisheria.

"Nataka niwapongeze wenzetu wa NSSF kwa kufanikisha kukamatwa kwa watuhumiwa hawa ambao wamekuwa wakifanya uhalifu wa kuuza maeneo ya NSSF na kuwadhulumu wananchi," alisema.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Malela, Oswin Mkinga, aliishukuru NSSF kwa kuweka mtego uliofanikisha kukamatwa kwa watuhumiwa hao na kuwa maeneo hayo yanamilikiwa na NSSF na ni sehemu ya mradi wa viwanja 20,000 vya Toangoma ambavyo vilinunuliwa kwa utaratibu wa fidia mwaka 2000.

Alisema kuanzia mwaka 2000 mpaka 2023, utaratibu uliratibiwa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa maana ya kuvipima na kuanza kuviuza.

Alisema kuanzia mwaka 2019 alipoingia kwenye uongozi wa mtaa huo, alikuta uvamizi wa viwanja hivyo lakini moja ya jitihada walizozifanya ni kutoa elimu kwa wananchi kuwa maeneo hayo ni mali ya NSSF na yanauzwa kwa utaratibu.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Masha Mshomba, Meneja Milki wa NSSF, Geofrey Timothy, alimshukuru Silaa kwa ushirikiano wake. Timothy alisema walipewa taarifa kuwa eneo hilo kuna matapeli wanashiriki kuuza maeneo ya mfuko, hivyo waliweka mtego uliofanikisha kukamatwa kwa watu hao.

"Ujumbe huu naomba ufike kwa wote waliovamia maeneo ya NSSF na pia ninawahakikishia wanachama wa NSSF kuwa maeneo yao yako salama kwa sababu tuna utayari wa kutosha wa kuyafanya yawe salama," alisema Timothy.

Mmoja ya wananchi waliotapeliwa kwa kuuziwa ardhi katika eneo hilo, Asha Ally Seif, aliipongeza NSSF kwa kufanikisha kukamatwa kwa watuhumiwa hao ambao wamekuwa wakitumia mbinu mbalimbali, ikiwamo kumtafuta bibi na kudai hilo ni eneo lake jambo ambalo ni kinyume cha sheria.



Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, SACP Jumanne Muliro, akionyesha kwa waandishi wa habari jana, silaha bandia aina ya bastola saba, AK 47 mbili yakiwemo mapanga na visu zilizokuwa zikitumiwa kutekeleza uhalifu pamoja na dawa za kulevya aina ya bangi puli 531, kete 2639, misokoto 158 na pikipiki mbili vilivyokamatwa katika operesheni maalum ya jeshi hilo, kuanzia Aprili mwaka huu. Watuhumiwa 13 wametiwa mbaroni katika operesheni hiyo. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Mbaroni tuhuma kutumia kusambaza dawa kulevya

Na Maulid Mmbaga

WATU 13 wakiwamo Hamis Seif (18), mkazi wa Mbondole na Bosco Bosco (18) mkazi wa Kipunguni, Ilala jijini Dar es Salaam, wamekamatwa kwa tuhuma za kuhusika na kuuza, kusafirisha na kutumia dawa za kulevya, ikiwamo bangi.

Kamanda wa Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Jumanne Muliro, alisema hatua hiyo ni mafanikio ya mwendelezo wa kusimamia mkakati maalumu wa kuzuia vitendo vya kihalifu mkoani humo.

Alisema watuhumiwa hao wamekamatwa na puli 531, kete 2,639, misokoto 158 ambayo ilikuwa tayari kutumiwa, viroba vinne vya bangi na pikipiki mbili zenye namba za usajili MC 673 CKM na MC 591 CUW zilizokuwa zinatumika kusambaza bangi.

"Katika hatua hiyo, Mei 21, mwaka huu, maeneo ya Kipunguni B, Ukonga, Jeshi la Polisi pia lilimkamata Hassan Yahya na wenzake watatu wakitumia dawa za kulevya aina ya bangi huku wakipanga njama za kufanya vitendo vya kihalifu, vikiwamo unyang'anyi.

"Watuhumiwa hao walikutwa na bastola bandia, AK47 mbili, majambia bandia mawili, mashoka mawili, kama sehemu ya maandalizi ya kufanya kuhalifu. Jeshi litaendelea kujikita katika kuzuia matukio ya kihalifu kwa kufuatilia kwa karibu makundi yote ya watu na hasa wanaotumia dawa za kulevya na kufanya matukio ya kihalifu," alisema.

Kamanda Muliro aliongeza kuwa katika usalama wa barabarani, jeshi linaendelea kuwafuatilia, kuwakamata na kuwafikisha mahakamani madereva wasiotii sheria na kanuni za usalama barabarani wakiwamo walevi na makosa hatarishi ya wapanda pikipiki za miguu miwili na miguu mitatu.

Pia alisema Aprili hadi Mei, mwaka huu, jumla ya makosa 67 ya pikipiki yalikamatwa yakihusisha kutokuwa na leseni, kuzidisha abiria na kuendesha pikipiki wakiwa wamelewa na madereva 21 walifikishwa mahakamani huku wengine walitozwa faini za papo hapo.

Pia alisema madereva wa magari sita walikamatwa kwa makosa ya kuendesha wakiwa wamelewa ambapo wawili walifikishwa mahakamani na wengine wanne walitozwa faini papo hapo.

Hata hivyo, alisema katika kipindi hicho, jeshi hilo katika kusimamia mifumo ya haki jinai lilifanikiwa kupata matokeo mahakamani ya watuhumiwa mbalimbali.

# Korti yatengua kaka kuwa msimamizi mirathi ya dada

Na Grace Gurisha

MAHAKAMA ya Rufani imesema yalikuwa makosa kwa Prof. William Kudoja kuteuliwa na Mahakama Kuu kuwa msimamizi wa mirathi ya marehemu dada yake, Salome Mbusa.

Imesema mahakama hiyo haikuzingatia kuwa mirathi hiyo haikumweka mume halali, Canisius Mbusa, kabla ya kufariki dunia mwaka 2015 baada ya uamuzi uliompa ushindi shemeji yake kutolewa.

Aidha, mahakama hiyo imeelekeza kuwa jalada la rufani hiyo, namba 133 ya mwaka 2021, lirudishwe Mahakama Kuu ili mchakato wa kumteua msimamizi wa mirathi, ambaye haegemei upande wowote uendelee.

Uamuzi huo ulitolewa jana na jopo la majaji watatu wa mahakama hiyo, Amour Khamis, Ignas Kitusi na Winfrida Korosso, baada ya kubaini kuwa Prof. Kudoja alipata uteuzi isivyo halali kutokana na kuficha taarifa muhimu.

Jopo hilo lilijiridhisha kuwa Marehemu Salome na mume wake Mbusa, hawakuwahi kutengana wala talaka haikuwapo na pia wamejiridhisha kuwa mali ambazo zilikuwa zimeorodheshwa zilikuwa zinamilikiwa na wanandoa hao.

Mali hizo ni nyumba iliyoko kiwanja namba 88, Barabara ya Guinea MS-OY 543, Oysterbay mkoani Dar es Salaam, magari matatu, ardhi, samani za ndani ya nyumba, fedha zilizokuwapo kwenye benki tatu na kiinua mgongo kutoka Benki Kuu ya Tanzania (BoT) alipokuwa akifanya kazi Salome.

Mahakama hiyo imeshangazwa na uamuzi uliotolewa na Jaji Edson Mkasimongwa ambao imesema si kwamba ulimwingiza usimamizi wa mirathi mume wa marehemu, Canisius Mbusa, lakini pia uliruhusu ombi la mirathi lililoletwa na kaka wa marehemu, kumteua Prof. Kudoja bila kuzingatia kuwa haikumweka mume halali kama mrithi wa mke wake. Kutokana na mgongano huo, mahakama imeona ni vyema akateuliwa Kabidhi Wasii Mkuu kama msimamizi wa mirathi hiyo ambaye haegemei upande wowote. Uamuzi huo ulisomwa na Naibu Msajili wa Mahakama hiyo, Wanjah Hamza.

Rufani hiyo ilikatwa na Julius Nkonya kwa niaba ya marehemu Canisius Mbusa kutokana na uamuzi wa Mahakama Kuu uliotolewa Desemba 15, 2015 wa kumteua Prof. Kudoja kuwa msimamizi wa mirathi kwa hoja ya kwamba wanandoa hao walikuwa wametengana na Salome aliacha urithi kwa baba yake, dada zake wawili na kwa kaka yake ( Prof. Kudoja).

Nkoya ambaye ni mrufani, aliwakilishwa na Wakili Aloyce Rugazia na mjibu rufani, Prof. Kudoja, aliwakilishwa na Wakili Daibu Kambo ambaye kwenye hoja zake alizozitoa, aliingiza mirathi na masuala ya mila na taratibu za kidini.

Baada ya Salome kufariki dunia Desemba 8, 2011 na kumuacha mume, Canisius Mbusa, Prof, Kudoja aliwasilisha maombi Mahakama Kuu kuwa msimamizi wa mirathi wakati shemeji yake bado alikuwa hai na mahakama ilikubaliana na ombi hilo.

# Nchimbi ataka wabadhirifu, wezi waombewe

**Na Romana Mallya,** KOROGWE

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, (pichani) amewataka Watanzania kuwaombea wenye roho za wizi, ubadhirifu ili ziwatoke.

Amesema haiwezekani Rais Samia Suluhu Hassan anahangaika kutafuta fedha ndani na nje ya nchi usiku na mchana na kuzishusha chini halafu hazitumiki kama ilivyokusudiwa.

Akizungumza jana na wananchi Korogwe, mkoani Tanga, Balozi Nchimbi alisema sehemu inayohitaji mifuko 10 ya saruji mtu anaweka miwili bila hata aibu.

Balozi Nchimbi ambaye yuko ziarani kutembelea mikoa mitano, aliwaomba Watanzania wamwombee Rais Samia kwa kuwa anaipenda nchi na kuitumikia kwa upendo na kujitolea kutafuta fedha, kuzisimamia zikusanywe sawasawa ili kujenga taifa.

Alisema Rais Samia anasimamia kutafuta fedha za mikopo na misaada kutoka nje na inashuka chini.

"Kuna baadhi ya viongozi Afrika ambao wakienda kuomba misaada au mikopo au kukusanya fedha, anagawana yeye na familia yake. Ziko nchi ambazo fedha za serikali kuu hazijawahi kufika chini miaka 20 imepita.

"Lakini Rais wetu anasimamia anasukuma zinakwenda kufanya kazi za maendeleo wajibu wetu ni kumwombea Rais wetu, ili aendelee kufanya kazi hii kwa upendo kama anavyofanya sasa, vilevile tuwaombee wasaidizi wake," alisema.



Nchimbi aliwataka wananchi wawaombee Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mikoa, Wakurugenzi na waandisi na wale wenye roho za wizi waombewe roho hizo zitoke.

### KUCHUNGA NDIMI

Akizungumza na wananchi wa Hedaru, mkoani Kilimanjaro, Balozi Nchimbi alisisitiza umoja na mshikamano wa taifa kwamba amani na utulivu vilivyopo havijaokotwa bali vimetengenezwa na kufanyiwa kazi na wazee na viongozi, wakiwamo waasisi wa taifa. Aliwakumbusha wananchi kuhusu kulinda amani ya nchi.

"Ninataka kusisitiza, kinachovuruga amani sehemu yoyote duniani ni ndimi zetu, kutochagua maneno ya kusema. Kuna watu wengine huwa wanasema kwanza halafu na kufikiri baadaye. Wengine wanafikiri kwanza ndipo wanasema," alisema.

Balozi Nchimbi aliwaomba viongozi wote wa siasa kutoka CCM na vyama vingine wanapotekeleza wajibu wao kwa jamii, wanapozungumza na wananchi, wawe wanafiriki kwanza kabla ya kutenda.

"Katika kila wanachosema tafakari maisha ya Watanzania, tafakari utakachosema kitachochea amani au kitachochea uvunjifu wa amani au kitaongeza mtengamano kwa watanzania.

"Wote wana CCM tushirikiane kuongea mambo ambayo hayawachanganyi Watanzania, hayawafarakanishi, hayawagombanishi ili nchi tuliyokabidhiwa na wazee wetu waasisi wetu na sisi tunakabidhi watoto na wajukuu zetu ikiendelea kuwa nchi yenye amani, upendo na mshikamano," alisema.

Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo CCM Taifa, CPA Amos Makalla, aliwaahidi wananchi kwamba watafanya ziara nyingine na kuzifika wilaya zote.

### DAWA ZA KULEVYA

Katika hatua nyingine, CCM imewaonya wauzaji wa dawa za kulevya kuwa wanapanda mbegu ya uharibifu katika taifa na kutoa wito kwa Watanzania kufanya kila linalowezekana kuachana na matumizi ya dawa hizo.

Balozi Emmanuel Nchimbi, alisema hayo juzi katika mkutano wa hadhara uliofanyika Mwanga, mkoani Kilimanjaro wakati wa ziara yake ya kutembelea mikoa mitano.

Nchimbi alisema changamoto kubwa ya wananchi wengi kujikita kwenye matumizi ya dawa za kulevya ambazo zinaua msingi wa ufanyaji kazi kwa vijana.

Alisema vijana wengi kwa sasa wapo kwenye matibabu ya matumizi ya dawa za kulevya na wao hawafiki asilimia 10 ya wale walioathirika.

"Ninaomba wazazi na viongozi wa dini wote mshiriki katika kazi ya kuhakikisha tunafanya kila linalowezekana watoto wetu wanakuwa watoto bora na waandaliwe kuja kulitumikia taifa.

"Njia moja ya kuwaandaa ni kuwapa mazingira mazuri ya na kuwatenganisha na uwezekano wa kuathirika na matumizi ya dawa za kulevya," alisema.

Balozi Nchimbi alitaka kila mwenye uwezo ambaye anajihusisha na dawa za kulevya ajue anapanda mbegu ya uharibifu katika taifa lake.

Pia alitaka kila mtu apate moyo wa uzalendo wa kulipenda taifa lake na kuacha vitu vinavyoleta madhara ya muda mrefu kwa taifa.


## Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com

**Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:**

1. Utafungua tovuti ya epaper.ippmedia.com utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza "subscribe"
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa kadi ya benki malipo kwa mtandao wa simu unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa namba ya simu unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. Kwa benki unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

**Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com**

6. Unafungua website yako ya www.ippmedia.com upande wa kulia utaona "E-Paper" utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian




Mwenyekiti wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC), Jaji Jacobs Mwambegele akizungumza wakati akifungua mkutano wa Tume na viongozi wa vyama vya siasa, jijini Dar es Salaam jana, ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura unaotarajiwa kuzinduliwa mkoani Kigoma, Julai 01, mwaka huu. **PICHA: INEC**

# Watu 11,900 kushiriki uchaguzi mdogo Kwahani

**Na Mwandishi Wetu**

WATU 11,936 wanatarajiwa kujitokeza kupiga kura kesho kwenye uchaguzi mdogo wa ubunge Jimbo la Kwahani, Wilaya ya Mjini, Mkoa wa Mjini Magharibi, Zanzibar.

Mwenyekiti wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC), Jaji wa Mahakama ya Rufani Jacobs Mwambegele, alisema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akisoma risala kwa ajili ya uchaguzi huo na kuongeza kwamba uchaguzi utahusisha vituo 29 vya kupigia kura.

"Jumla ya wapigakura 11,936 walioandikishwa katika Daftari la Kudumu la Wapigakura la Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC) watashiriki katika uchaguzi huu mdogo na jumla ya vituo 29 vya kupigia kura vitatumika," alisema.

Wagombea wanaowania kiti cha ubunge Kwahani majina yao na vyama katika mabano ni Bashir Yatabu Said (Demokrasia Makini), Nuru Abdulla Shamte (DP), Mwanakombo Hamad Hassan (NLD), Zainab Maulid Abdallah (CCK), Tatu Omary Mungi (UPDP), Khamis Yussuf Mussa (CCM) na Jarade Ased Khamis (AAFP).

Wengine ni Kombo Ali Juma (NRA), Shara Amran Khamis (ADC), Naima Salum Hamad (UDP), Madina Mwalim Hamad (ADA TADEA), Amour Haji Ali (SAU), Mashavu Alawi Haji (UMD) na Abdi Khamis Ramadhan (CUF).

Jaji Mwambegele alivikumbusha vyama vya siasa, wagombea, mawakala wa vyama, wapigakura na wananchi kwa ujumla kuhakikisha hawapigi kampeni siku ya kupiga kura kwa kuwa kufanya hivyo ni kinyume cha sheria.

"Alama za vyama vya siasa zinazoashiria kampeni kama vile vipeperushi, bendera na mavazi haviruhusiwi kutumika kesho tarehe 08 Juni, 2024 ambayo ni siku ya uchaguzi," alisema. Jaji Mwambegele aliongeza kwamba kazi ya kupiga kura katika maeneo yote ya uchaguzi, itafanyika katika vituo vilivyotumika wakati wa uchaguzi mkuu wa mwaka 2020. Aliongeza kwamba vituo vya kupigia kura vitafunguliwa saa 1:00 asubuhi na kufungwa saa 10:00 jioni.

"Iwapo wakati wa kufunga kituo watakuwapo wapigakura katika mstari ambao wamefika kabla ya saa 10:00 jioni katika mstari na hawajapiga kura, wataruhusiwa kupiga kura. Mtu yeyote hataruhusiwa kujiunga katika mstari wa wapigakura baada ya saa 10:00 jioni," alisema. Jaji Mwambengele alibainisha kwamba watakaoruhusiwa kupiga kura ni wale tu ambao walioandikishwa katika Daftari la Kudumu la Wapigakura la Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC).

Alisema tume imeandaa majalada ya nukta nundu katika vituo vya kupigia kura kwa ajili ya kuwawezesha watu wenye ulemavu wa kuona kupiga kura bila usaidizi.

Pia alisema wapigakura wenye ulemavu wa kuona ambao hawawezi kutumia majalada hayo, wataruhusiwa kwenda vituoni na watu watakaowachagua wenyewe kwa ajili ya kuwasaidia kupiga kura.

"Katika kituo cha kupigia kura, kipaumbele kitatolewa kwa wagonjwa, watu wenye ulemavu, wazee, wajawazito na akina mama wanaonyonyesha watakaokwenda na watoto kituoni," alisema.

Kuhusu wapigakura kurudi nyumbani baada ya kupiga kura, Jaji Mwambegele alisema hilo ni sharti la kisheria na kwamba maadili ya uchaguzi yaliyotiwa saini na kuridhiwa na vyama vyote vya siasa, serikali na tume yanaelekeza hivyo. "Wapigakura watatakiwa kuondoka kituoni mara wanapomaliza kupiga kura ili kuepusha msongamano na vitendo vinavyoweza kuchochea uvunjifu wa amani. Tume inawashauri wananchi kujiepusha na mikusanyiko katika maeneo ya vituo vya kupigia kura," alisisitiza.

Alitoa rai kwa wapigakura katika Jimbo la Kwahani kujitokeza kwa wingi kwenye vituo vya kupigia kura ili kuwachagua viongozi wanaowataka.

# Hasara bil. 100/- uchomaji moto misitu

**Na Elizabeth John,**
WANG'INGO'MBE

MKUU wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, amesema mkoa huo umepata hasara zaidi ya Sh. bilioni 100 kwa kipindi cha miaka mitatu kutokana na uchomaji wa moto kwenye misitu.

Mtaka aliyasema hayo juzi wakati wa maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani yaliyofanyika kimkoa katika kijiji cha Itengelo, kata ya Saja, wilaya ya Wang'ing'ombe.

Alisema wakati NEMC ikipambana na kukabiliana na uharibifu wa mazingira, ni lazima hatua mbalimbali ziendelee kuchukuliwa dhidi ya moto kichaa.

"Tumezielekeza mamlaka za serikali za vijiji kutunga sheria ndogo ndogo ya kuadhibu uchomaji ovyo wa maeneo yao kwa sababu moto unatokana na usafishaji wa mashamba. Mtu anasafisha shamba lake, mabua ya mahindi na moto unamshinda unashika shamba la miti unateketeza maekari ya miti," alisema.

Mtaka alisema pia wameelekeza serikali za vijiji kusimamia vyanzo vyote vya maji kwamba miti inayopandwa iwe rafiki sambamba na kulindwa na kutunzwa ili kupata faida mbili miti na maji.

Awali, Meneja wa Baraza la Taifa na Hifadhi na Usimamizi Mazingira (NEMC) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Josiah Muruny,a alisema kila mmoja anapaswa kulinda mazingira kwa kuhifadhi vyanzo vya maji na ndio maana wanaendelea kukapanda miti aina ya mivengi ambayo ni rafiki na vyanzo vya maji.

Alisema zaidi ya miti 1,000 imepandwa katika maeneo mbalimbali wilayani Wanging'ombe ili kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

"Mkoa wa Njombe umekuwa ni moja ya mikoa ambayo inasimamia suala la ulinzi wa mazingira pamoja na kuhimiza wananchi kupanda miti ambayo ni ya matunda," alisema Murunya.

Wananchi wa kijiji cha Itengelo mbali na kupongeza jitihada za utunzaji mazingira lakini wameiomba serikali kuwasaidia kutatua kero mbalimbali zinazowakabili zikiwamo za migogoro ya ardhi.

"Suala linasumbua sana sisi ni mipaka, mpaka wa Itengolo na Makambako ambao wanatuingilia sehemu ambayo sio ya kwao kila tukilalamika tatizo hili haliishi," alisema

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe, Agnetha Mpangile, alisema wilaya hiyo inaendelea kutatua migogoro ambayo imekuwa ikisababisha madhara kwa wananchi.

"Kikubwa katika kata hii mh Mkuu wa Mkoa ni migogoro ya mipaka hili jambo hata sisi tulipokuwa huku ziara tumelisikia, naomba ulichukue kwa umakini na uharaka linaweza hata kuathiri uchaguzi," alisema Mpangile.

# Waonywa mikopo ya kausha damu

**Na Mwandishi Wetu,**
SUMBAWANGA

SERIKALI imetoa rai kwa wananchi kuepuka kukopa fedha kwenye vikundi vinavyotoa huduma za kifedha bila kusajiliwa rasmi kwa mujibu wa sheria ili kuepuka athari zinazoambatana na mikopo umiza.

Ofisa Msimamizi wa Fedha kutoka Wizara ya Fedha, Jackson Mshumba, alitoa rai hiyo juzi wakati wa semina ya masuala ya fedha iliyofanyika katika Manispaa ya Sumbawanga mkoani Rukwa.

"Tumekuja kubaini kwamba wananchi wengi wako katika vikundi ambavyo havijasajiliwa rasmi kwa mujibu wa Sheria ya Huduma Ndogo ya Fedha ya mwaka 2018. Kwa hiyo nitoe rai kwa wananchi ni vyema wakawa na mwamko wa kujiunga katika vikundi ambavyo ni rasmi na vimesajiliwa kwa mujibu wa sheria hiyo," alisema.

Mshumba alisema serikali inaendelea na program ya utoaji elimu vijijini husussan kwa mkoa wa Rukwa na wananchi wamepata elimu wanavyoweza kuwa na nidhamu ya kujiwekea akiba lakini pia wamepata uelewa juu ya mikopo umiza ili kuepukana na changamoto hii kwa sasa ya mikopo kausha damu.

Alisema katika mwendelezo wa program hiyo, imebainika kuwa wananchi wengi hawana uelewa wa masuala ya mikopo, taratibu za mikopo hawazifahamu lakini pia wananchi wengi hawafahamu masharti yaliyoko katika mikopo wanayochukua kwa watoa huduma mbalimbali.

Mshumba aliongeza kwa kuwasisitiza wananchi kuwa kabla ya kuchukua mikopo ni vyema wakajiridhisha kuhusu suala la riba, kama mtoa huduma amesajiliwa kwa mujibu wa sheria na pia waelewe vigezo na masharti yaliyopo kwenye mkataba husika.

Alitoa rai kwa wananchi kwa kuwaomba endapo watabaini kwamba kuna vikundi vidogo vya huduma ndogo ya fedha vipo mitaani na havijasajiliwa watoe taarifa kwa mamlaka husika ambazo ni pamoja na maofisa maendeleo ya jamii kwenye mamlaka za wilaya na mikoa.

Awali, mkazi wa kijiji cha Kaengesa, Wilaya ya Sumbawanga, Rehema Lukali, alisema ujio wa wataalamu kutoka Wizara ya Fedha umewafungua macho kuhusiana na akiba kwamba ili kuaminika katika vyombo vya fedha, lazima mtu awe mwanachama na chama chake kiwe kimesajiliwa kisheria. Naye Mishek Kassian ambaye pia ni mwanakikundi wa Kambarage kilichoko katika kijiji cha Lyapona, wilaya ya Sumbawanga, alisema kupitia elimu aliyoipata, amejifunza mengi na atawaelimisha watu wengine kwa kuwa anaona mikopo mingi inatolewa na watu binafsi na taasisi mbalimbali huku wengi wakikopa bila kuwa na malengo.



Katibu Tawala wa mkoa wa Kigoma, Hassan Kaigwa, akitoa elimu kwa wananchi kuhusu masuala ya hati fungani mbalimbali zinazouzwa na Serikali, ili iwe moja ya vyanzo vya kujiongezea vipato badala ya kuweka fedha zao katika mifumo isiyo rasmi, wakati wa semina iliyofanyika mjini Kigoma, mapema wiki hii. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# Aliyefungwa maisha kwa kubaka aachiwa

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA ya Rufani Tanzania imemwondolea adhabu ya kifungo miaka 30 jela, kifungo cha maisha na fimbo 12 Zilam Hamisi, aliyehukumiwa kwa kubaka na kuwalawiti wanafunzi wawili.

Hatua hiyo imetokana na mahakama kubaini upungufu katika ushahidi wa upande wa Jamhuri.

Mahakama hiyo mbele ya jopo la majaji Barke Sehel, Panterine Kente na Gerson Mdemu, ilitoa hukumu hiyo jana baada ya kupitia hoja za kupinga adhabu zilizowasilishwa na mrufani.

Wakati ukisomwa uamuzi huo, Mahakama ilisoma ushahidi uliotolewa katika shauri lililodaiwa Oktoba 5, 2018 kwamba baada ya saa za shule, wasichana wawili wa shule ya msingi wenye umri wa miaka 11 na 12 walikuwa wamesimama kwenye kituo cha mabasi cha Mzambarauni, wakisubiri basi linalokwenda nyumbani kwao, Gongo la Mboto.

Inadaiwa kwenye kituo hicho, kulikuwa na mtu aliyesimama nyuma ya wanafunzi hao huku akizungumza kwenye simu yake ya mkononi na kisha akawauliza wasichana wanasoma shule gani.

Wanafunzi hao walimjibu kwamba walikuwa wanafunzi wa darasa la sita katika Shule ya Msingi Mzambarauni kisha wakasikia mwanamume akimwambia mtu huyo kwa simu kwamba amewapata wasichana hao wawili.

Mwanamume huyo inadaiwa alikata simu na kuwaambia kuwa alielekezwa na mwalimu mkuu wao kuwachukua hadi maktaba ya Chanika Mbande na Mbagala kukusanya vitabu vya shule.

Mtu huyo inadaiwa akaendelea kuongea na simu akijifanya anazungumza na mwalimu wao mkuu, walimsikia akizungumza kuwaombea ruhusa kwa wazazi wao. Inadaiwa kuwa baada ya kukata simu, aliwahakikishia wasichana wasiwe na wasiwasi kwani wazazi wao tayari wamempa ruhusa ya kwenda nao maktaba.

Wanafunzi hao wanadaiwa walimwamini, wote watatu walipanda basi la kwenda Chanika Mwisho. Baada ya kufika huko, yule mtu akawaambia wamfuate, walilazimika kumfuata, walitembea kwa muda mrefu kwa miguu hadi msituni.

Inadaiwa wakiwa msituni, mtu huyo alidanganya wasichana kwamba msitu ulikuwa unalindwa na askari, hivyo, wanapaswa kumruhusu kufunga mikono yao kwa kamba ili askari wakitokea angejifanya amewakamata.

Watoto waliamini na kumwacha afunge, alitaka kufunga miguu yao lakini walipinga ndipo alipotishia kuwaua iwapo wasingemruhusu kufunga miguu yao.

Inadaiwa aliwafunga miguu, akawavua nguo na alianza kuwabaka na kuwalawiti, mmoja baada ya mwingine baada ya kutimiza lengo lake akawarudisha wasichana Chanika na kuwaacha wakiwa hoi.

Wazazi wao walipata wasiwasi walianza kutafuta lakini usiku wa manane, wasichana walipata njia ya kurudi nyumbani wakiwa na hali mbaya kwani walikuwa wamepakwa kinyesi juu ya nguo.

Inadaiwa walisimulia yote kwa wazazi wao, wazazi walipeleka suala hilo katika Kituo cha Polisi cha Gongo la Mboto kisha waathiriwa walipelekwa katika Hospitali ya Amana kwa uchunguzi wa kimatibabu.

Daktari wa Amana, Magreth Ibobo, ambaye aliwafanyia uchunguzi, alibaini wanafunzi walifanyiwa ukatili huo kwa kuwa sehemu zao za siri zilikuwa wazi.

Askari Polisi wa Kituo cha Polisi cha Stakishari waliweka mtego ili kunasa mkosaji ambapo mrufani alikamatwa Oktoba 10 mwaka 2018 katika Kituo cha basi cha Mzambarauni akiwa na watoto wengine aliodaiwa kutaka kuwapeleka msituni Chanika.

Mrufani alishtakiwa katika Mahakama ya Wilaya ya Ilala na kufunguliwa mashtaka manne yakiwemo mawili ya kubaka na mawili ya kuingia kinyume na maumbile.

Katika usikilizwaji alijitetea mwenyewe hakuwa na shahidi na mwisho wa shauri Mahakama ilimtia hatiani na kumuhukumu kwenda jela miaka 30 kwa makosa ya kubaka na kifungo cha maisha kwa makosa ya kulawiti.

Pia aliamuliwa kulipa faini ya Sh 200,000 kwa kila kosa la kubaka na fidia ya Sh 300,000 kwa kila kosa la kulawiti, pia achapwe fimbo tatu kwa kila kosa.

Mrufani alipinga adhabu hizo akiwa na sababu mbalimbali ikiwemo Mahakama ilikosea kumtia hatiani wakati Jamhuri haikuthibitisha mashtaka dhidi yake, ushahidi wa shahidi wa kwanza na wapili ulikuwa wa uongo na si wa kuaminika.

Upande wa Jamhuri uliwakilishwa na Wakili Michael Lucas akisaidiana na Jenina Rugalama.

Baada ya Mahakama kusikiliza rufani hiyo, ilibaini kulikuwa na mkanganyiko na kwamba shahidi wa kwanza na wapili walishindwa kutoa maelezo ya kina ya aliyewafanyia tukio hilo.

"Tulishindwa kupata uhusiano wowote kati ya kukamatwa kwa mrufani Oktoba 10, 2018 na tukio lililotokea Oktoba 5,2018. Vile vile shahidi wa tano aliaminiwa na mahakama mbili za chini kwamba mrufani alikamatwa akiwa anakaribia kutenda kosa kama hilo lakini afisa wa polisi, Koplo Emmanuel ambaye alimkamata mrufani hakuitwa kama shahidi.

"Kwa kuwa afisa aliyekamata hakuitwa kutoa ushahidi kwa sababu zisizojulikana, tunalazimika kuona kulikuwa na upungufu kwa upande wa mashtaka kwani angekuwa ameitwa ingetoa mwanga juu ya sababu halisi ya kukamatwa kwa mrufani," lilisema jopo.

Baada ya kusema hayo Mahakama ilifuta hukumu na kuondoa amri za malipo ya faini na fidia na fimbo ikiwa bado haijatekelezwa.

Mahakama ilitoa agizo la kuachiliwa mara moja kwa Hamis, isipokuwa kama anashikiliwa kihalali kwa madhumuni mengine yoyote halali.

# TPDC yabuni mbinu kumaliza uhaba mafuta

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) linatarajia kujenga matangi sita ya kuhifadhi mafuta yenye tani za ujazo wa lita 162,000 yatakayosaidia taifa kuwa na akiba kubwa ya mafuta.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya TPDC, Balozi Ombeni Sefue, alisema hayo jana Dar es Salaam wakati bodi hiyo ilipotembelea Kampuni ya Kuhifadhi Mafuta Tanzania (TIPER) lengo likiwa kukagua tangi namba nane lililokuwa linahifadhi mafuta pamoja na kuangalia shughuli zingine zinazoendelea eneo hilo.

"Tangi namba nane ni la muda sana tangu mwaka 1993 lakini mwaka 2000 lilifungwa baada ya kuingia kwa soko huria kutokana na kutoleta faida kwa taifa. Mojawapo ya maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan kwa TPDC ni kuhakikisha taifa linakuwa na akiba ya mafuta. Hiyo ndiyo sababu imetusukuma kuja kutembelea hapa TIPER," alisema Balozi Sefue.

Alisema tangi hilo namba nane litafufuliwa na mchakato wake utachukua muda wa miezi 20 ili lianze kuhifadhi mafuta.

"Ifikapo mwanzoni mwa mwaka 2026 mchakato wa kuanza ukarabati utakuwa unaanza kwa sababu kila kitu kimeshakamilika ikiwemo kuanza kutangaza zabuni," alisema.

Balozi Sefue alisema katika kuhakikisha taifa linakuwa na akiba kubwa ya mafuta, TPDC inatarajia kujenga matangi mengine sita na kwamba zabuni ya kupata makandarasi itafunguliwa muda wowote mwezi huu.

Meneja wa Biashara ya Mafuta TPDC, Baraka Nyakutonya, alisema hadi sasa kuna kampuni kadhaa ambazo zimeonyesha nia ya kuomba zabuni ya ukarabati wa tangi namba nane.

Alisema Juni 17, mwaka huu, zabuni itatangazwa ili kampuni zianze kuomba na taratibu zingine ziendelee.

Nyakutonya alisema tangi hilo linauwezo wa kuhifadhi mafuta metriki tani 46,000.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# TFF iangalie tena utoaji tuzo

**NI** wiki mbili sasa tangu Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2023/2024 kumalizika ukishuhudia Yanga wakitangazwa ubingwa , Azam wakikata tiketi ya kushiriki Ligi ya Mabingwa Afrika, Coastal Union wakiungana na Simba kucheza Kombe la Shirikisho Afrika.

Baada ya Ligi hiyo kumalizika pia ni wiki imepita tangu kuchezwa mchezo wa fainali ya Kombe la FA la CRDB na kushuhudia Yanga wakitetea tena ubingwa wao.

Baada ya matukio hayo, tukio kubwa lililobaki kuhitimisha kabisa matukio ya msimu huo ni utoaji wa tuzo kwa wachezaji bora katika msimu uliopita.

Kwa kawaida tuzo hizo zilikuwa zikitolewa wiki moja tu baada ya kufanyika kwa fainali ya Kombe la FA, lakini kwa msimu huu TFF imetangaza ratiba tofauti.

Kwa mujibu wa TFF, imetangaza tuzo hizo kutolewa wakati wa michuano ya Ngao ya Jamii ambapo kilele chake kitaendana na utoaji wa tuzo hizo.

Inawezekana kukawa na malengo mazuri tu katika kuweka ratiba hiyo ya utoaji wa tuzo kwa wanasoka bora kwa msimu uliopita, lakini sisi Nipashe tuna mtazamo na ushauri tofauti juu ya utoaji wa tuzo hizo.

Ikumbukwe wachezaji wengi wanapata mapumziko baada ya mashindano kumalizika, hii inamaana baada ya mchezo wa fainali ya kombe la FA wachezaji wanaingia kwenye kipindi cha mapumziko.

Kwa mfano, uongozi wa Yanga tayari umetangaza kuwapa mapumziko wachezaji wake mpaka mwezi Julai watakapokutana tena kwa ajili ya maandalizi ya mismu mpya.

Ni kweli msimu mpya uwa unaanza mwezi Agosti na hivyo wachezaji wote wanakuwa wamerejea kwenye tyimu zao, hata hivyo wapo wachezaji ambao wanaweza wakasajili na timu nyingine nje ya nchi hususani wale wa kimataifa na kupelekea kukosa kuhudhuria hafla ya tuzo hizo.

Uzuri na kuchangamka kwa sherehe za utoaji tuzo inapaswa wachezaji husika kuwepo na kupokea wenyewe tuzo zao.

Hapa ndipo tunaposhauri TFF kurejesha utaratibu wa kutoa tuzo katika kipindi kile kile cha angalau wiki moja au mbili baada ya msimu kumalizika ili kuweza kuwa na wachezaji wote waliostahili au waliochaguliwa kupewa tuzo.

Tulishuhudia msimu uliopita, baadhi ya wachezaji wakubwa walioteuliwa kupewa tuzo hawakuwepo na kutuma wawakilishi, hii inapunguza radha ya tukio zima.

Wazo la kufanya sherehe za tuzo mwishoni mwa michezo ya Ngao ya Jamii sio mbaya, lakini liangaliwe upya ili kuweza kuwa na uhakika wa kuwa na nyota wote wanaopaswa kupewa tuzo hizo.

Lingine TFF tunaomba mboreshe tukio zima la utoaji tuzo liendani na ukubwa wa Ligi yetu, wachezaji waone kweli jasho na vipaji vyao vinathaminiwa.

Msimu uliopita mmetuthibitishia umakini wetu kwenye kusimamia kanuni na kuhakikisha Ligi inachezwa kwa ushindani na kwa uwazi mkubwa, ili limefanikiwa kiasi kikubwa ingawa yapo makosa madogo madogo.

Sasa tunaomba na hili la tuzo mtuonyeshe kuwa mmejipanga na mmebadilika , tunatarajia tukio la aina yake kwenye utoaji wa tuzo, liendane na ubora wa ligi yetu ambayo kwa sasa imekuwa kivutio kikubwa kwa wachezaji kutoka nje ya nchi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

Na Adam Fungamwango

# Kanuni za 'play off', ushirikina Ligi Kuu hazifai, zibadilishwe

**TAYARI** Bodi ya Ligi Kuu imeanza kupokea maoni kwa ajili ya maboresho ya kanuni za Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2024/25.

Ofisa Habari na Mawasiliano wa Bodi hiyo, Karim Boimanda, akasema tayari wameshaanza kupokea maoni kwa njia mbalimbali za mawasiliano, huku akiahidi kuwatembelea pia wadau wa soka, vikiwemo vyombo vya habari kwa ajili ya kupata mawazo mengi zaidi yatakayofanya kuwe na kanuni bora msimu ujao.

Hata hivyo, alikiri kuwa eneo la imani za kishirikina ndilo lililoonekana kuvutia wadau wengi kutoa maoni yao kuliko kanuni zingine.

"Tumeanza kupokea maoni, lakini ukweli kabisa nikiri kanuni iliyovunjwa sana msimu huu ni ile inayozungumzia imani za kishirikina, na ndiyo inayotolewa maoni mengi kwa sasa na wadau kuliko zingine kuonyesha ni namna gani hawaridhishwi na adhabu zinazotolewa, wanasema haizuii au haiwatishi watu kuendelea na tabia hiyo," alisema Boimanda.

Binafsi, kwanza niwapongeze Bodi ya Ligi kwa kuwa na wazo la kuwatembelea wadau walipo, wakiwemo wanahabari kwa ajili ya kupata maoni mengi na kwa karibu zaidi huku akishuhudia hisia za wadau wenyewe.

Kabla hata hawajatembelea vyombo vya habari, binafsi naanza kabisa kutoa maoni yangu kama mmoja wa wadau wa soka nchini.

Kwanza kabisa ni kuhusu kanuni ya ushirikina, ni kosa ambalo limekuwa likijirudia kama ambavyo bodi yenyewe ilivyobainisha.

Hata mimi siridhishwi na adhabu za faini zinazotolewa, ambazo klabu hazishtuki, badala yake zinarudia mechi baada ya mechi huku taarifa zikisema hata hizo faini zenyewe hukatwa kwenye viingilio vya mechi.

Kwangu ningependa iwekwe kanuni ya kuzikata pointi mbili timu zinazothibitika kufanya kosa hilo.

> **Pointi mbili tu, zinatosha kuitoa timu kwenye reli na isirudie tena mchezo huo, na ikiwezekana iwe pointi na faini juu ili kutokomeza kabisa vitendo hivyo vya aibu kwenye soka letu.**

Pointi mbili tu, zinatosha kuitoa timu kwenye reli na isirudie tena mchezo huo, na ikiwezekana iwe pointi na faini juu ili kutokomeza kabisa vitendo hivyo vya aibu kwenye soka letu.

Ila angalizo ni kwamba timu isikatwe kama vitendo hivyo vinafanywa na mashabiki, kwa sababu timu zinaweza kuhujumiana.

Mashabiki wa timu pinzani wanaweza kwenda katika mechi ya wenzao na kuvaa jezi za wapinzani wao na kuonyesha vitendo hivyo ili tu kuiponza timu husika.

Adhabu itolewe kwa makosa ya viongozi, wachezaji na watu ambao wanajulikana kuwa wapo ndani ya klabu husika.

Ukakasi mwingine ni kuhusu mechi za mchujo.

Ki ukweli mechi hizi zimekuwa nyingi sana kiasi cha kuwachanganya hata mashabiki na hazitendi haki kwa timu za madaraja ya chini.

Mimi sikatai 'play off', lakini iwe moja tu, yaani timu mbili za chini katika Ligi Kuu, zitakazoshika nafasi ya 16 na 15 zishuke moja kwa moja, itakayoshika nafasi ya 14 iende moja kwa moja kucheza na timu itakayomaliza nafasi ya tatu Ligi ya Championship, baada ya zile mbili za juu kupanda.

Kuwa na 'play off' nne, yaani wa Ligi Kuu wenyewe, Champioship nao wawe na mechi yao alafu washindi waje kukutana ni mlolongo mrefu. Bodi ya Ligi tunaomba ifanyie kazi ushauri huu

**HABARI KITAIFA**

# Vyama ruksa kuweka mawakala uboreshaji daftari wapigakura

**Na Mwandishi Wetu**

VYAMA vya siasa vitaruhusiwa kuweka wakala mmoja kwenye kila kituo cha kuandikisha wapigakura kwenye uboreshaji wa Daftari la Kudumu la WapigaKura unaotarajiwa kuzinduliwa Julai Mosi mkoani Kigoma.

Mwenyekiti wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC), Jaji wa Rufani Jacobs Mwambegele, aliyasema hayo jana wakati akifungua mkutano wa tume na viongozi wa vyama vya siasa uliofanyika Dar es Salaam ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya uboreshaji wa daftari.

"Leo (leo) kila chama kitapewa nakala ya orodha ya vituo vyote vya kuandikisha wapigakura. Lengo la kuwapatia nakala hizo ni kuwawezesha kupanga na kuweka mawakala wa uandikishaji katika vituo vya kuandikisha wapiga kura.

"Kila chama kitaruhusiwa kuweka wakala mmoja kwenye kituo cha kuandikisha wapigakura kwa lengo la kushuhudia utekelezaji wa uboreshaji kituoni ikiwamo kuwatambua wale wanaokuja kituoni kama wana sifa za kuandikishwa," alisema.

Jaji Mwambegele alisema kwamba kikao hicho ni sehemu ya utamaduni wa tume iliojiwekea wa kuwashirikisha wadau wa uchaguzi wakati wa utekelezaji wa majukumu yake.

Aliwataja wadau hao kuwa ni pamoja na viongozi wa vyama vya siasa, viongozi wa dini, wawakilishi wa asasi za kiraia, wahariri wa vyombo vya habari, waandishi wa habari, maofisa habari wa mikoa na halmashauri, wawakilishi wa makundi mbalimbali ya vijana, watu wenye ulemavu na wanawake.

"Niwaombe viongozi wa vyama vya siasa kwa umoja wenu kuzingatia sheria za uchaguzi, kanuni za uboreshaji na maelekezo ya tume kuhusu uboreshaji wa daftari. Tume kwa upande wetu tutazingatia Katiba, sheria ya uchaguzi na kanuni zilizotungwa chini ya sheria katika uboreshaji," alisema.

Mkurugenzi wa Uchaguzi wa INEC, Ramadhani Kailima, alisema pamoja na kufanyika kwa uzinduzi Julai Mosi, ambapo mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, uboreshaji wa daftrai utaanza siku hiyo mkoani Kigoma na kuendelea kwa siku saba hadi Julai 7, mwaka huu.

"Kwa lengo la kutekeleza jukumu hilo kwa ufanisi, uboreshaji utafanyika kwenye mizunguko 13 itakayobainishwa kwenye ratiba. Aidha, zoezi hili litaendeshwa kwa siku saba kwenye kila kituo cha kuandikisha wapigakura," alisema.



Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Dk. Ashura Katunzi (wa pili kulia), akizungumza wakati wa ufunguzi wa mjadala wa usalama wa chakula, jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni Kaimu Mkurugenzi wa Uendelezaji Viwango, Bahati Samilani (kushoto) na Ofisa Biashara Mwandamizi Wizara ya Viwanda na Biashara, Festo Kapela (wa pili kushoto) na Kaimu Mkurugenzi wa Udhibiti Ubora TBS, Amina Kitindi. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# TBS yataka usalama mnyororo uzalishaji chakula

**Na Joseph Mwendapole**

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS), limesema kuna umuhimu kwa wafanyabiashara wa mnyororo wa chakula nchini kuimarisha mifumo ya uzalishaji ili kuhakikisha uzalishaji wa chakula salama na kukabiliana na vihatarishi vya usalama wa chakula.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TBS, Dk. Ashura Katunzi, wakati wa mjadala wa maadhimisho ya Siku ya Chakula Salama Duniani.

Alisema serikali kupitia taasisi zake imekuwa na mipango ya kukabiliana na vihatarishi vya usalama wa chakula na kuimarisha mfumo wa udhibiti wa usalama wa chakula, ikiwa ni pamoja na kuongeza ufuatiliaji na uratibu wa masuala mtambuka na kuimarisha mawasiliano kati ya serikali, wafanyabiashara wa chakula na jamii kwa ujumla.

"Chakula salama ni jukumu la kila mmoja, hivyo natoa wito kwa kila mdau kushiriki kikamilifu katika mdahalo huu, kujadili jinsi kila mdau alivyojiandaa katika kukabiliana na dharura zitokanazo na uchafuzi wa chakula au madhara yatokanayo na ulaji wa chakula kisicho salama," alisema.

Alisema kila mmoja katika nafasi yake analo jukumu la kufanya tathmini kuhusu vihatarishi vinavyoweza kusababisha uchafuzi wa chakula na madhara yake, pamoja na kuweka miundombinu ya kukabiliana na hali hiyo endapo ikitokea.

Dk. Katunzi alisema walaji nao wanalo jukumu la kuelewa vihatarishi vya usalama wa chakula na mazingira yanayosababisha uchafuzi wa chakula, madhara yatokanayo na kula chakula kisicho salama, kutoa taarifa juu ya chakula kisicho salama, pamoja na kufahamu namna ya kukabiliana na matukio yatokanayo na ulaji wa chakula kisicho salama.

Alisema kaulimbiu ya maadhimisho ya Siku ya Chakula Salama Duniani kwa mwaka huu 'Chakula Salama: Jiandae kwa Usiyoyatarajia', inatahadharisha juu ya umuhimu wa kujiweka tayari wakati wote kukukabiliana na vihatarishi inayoweza kuathiri usalama wa chakula na pia utayari wa kukabiliana na madhara yatokanayo na chakula kisicho salama

"Kwa mantiki hiyo, wadau tunahimizwa kujenga uwezo katika kuzuia, kung'amua na kukabiliana na dharura zitokanazo na chakula kisicho salama kwani madhara ya chakula kisicho salama ni makubwa, ikiwemo madhara ya kiafya na kiuchumi, ikiwemo kushindwa kumudu katika biashara ya ushindani," alisema.

Kwa mujibu wa Dk. Katunzi, ulaji wa chakula kisicho salama umehusishwa na magonjwa mbalimbali, pamoja kusababisha changamoto nyingine za kiafya kama vile ukuaji duni kwa watoto, hali duni ya lishe kwa wakubwa na watoto, pamoja na kuongezeka kwa magonjwa yanayoambukiza na yasiyoambukiza.

Pia alisema kwa mujibu wa takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO) inakadiriwa kuwa kila mwaka mtu mmoja katika kila watu 10, huugua kutokana na ulaji wa chakula kisicho salama duniani na kuwa watu 420,000 kati ya wanaougua hufariki dunia.

"Madhara haya ni makubwa zaidi katika nchi zinazoendelea, na waathiriwa wakubwa wakiwa ni watoto walio chini ya miaka mitano kwa hiyo kwa pamoja bado tuna kazi kubwa ya kufanya kwenye usalama wa chakula," alisema Dk. Katunzi.

Alisema maadhimisho ya Siku ya Chakula Salama Duniani hufanyika kila Juni 7 na kwamba pamoja na kuongeza uelewa wa jamii juu ya masuala ya chakula salama na kufikisha ujumbe kwa wadau mbalimbali kuhusu kuzuia magonjwa yatokanayo na chakula kisicho salama, na kutoa fursa ya majadiliano kuhusu mbinu shirikishi kukabiliana na uchafuzi wa chakula.

Ofisa Biashara Mwandamizi wa Wizara ya Viwanda na Biashra, waFesto Kapela, alisema usalama wa chakula ni mnyororo mrefu na kila mdau anatakiwa kutimiza wajibu wake ili kuhakikisha chakula hakisababishi madhara kiafya kwa watumiaji.

"Kwenye mnyororo mzima wa chakula bado Tanzania hatujafikia pazuri kwa hiyo wadau mnaoshiriki kwenye mjadala huu wa leo mnapaswa kutoa maoni yenu kuhakikisha suala la usalama wa chakula linasimamiwa ipasavyo," alisema.

## Wanafunzi wasisitizwa kusoma masomo sayansi

**Na Mary Geofrey**

SERIKALI imewataka wanafunzi kujikita kwenye masomo ya sayansi ili taifa lizalishe wataalamu wa kutosha wenye kutoa majibu ya dunia.

Aidha, wazazi wametakiwa kutambua wajibu wao wa kwanza katika kuzalisha wanasayansi wa kutosha kupitia malezi bora yanayoanzia nyumbani.

Katibu Mkuu, Wizara ya Afya, Dk. John Jingu, alitoa rai hiyo jana jijini Dar es Salaam, katika hafla ya kutoa zawadi kwa wanafunzi 34 na walimu sita waliofanya vizuri kwenye masomo ya sayansi wa kidato cha nne na sita mwaka 2022/23.

"Sayansi kazi yake ni kutafuta majabu ya matatizo ya kina na siyo ya kufikirika lakini ni vizuri kutafuta majawabu ya changamoto kubwa zinazoikumba dunia, kupitia wanafunzi ambao leo tunawaandaa kupitia masomo ya sayansi," alisema Dk. Jingu.

Aliwataka wanafunzi hao kutumia dhana za kisayansi kupata majibu sahihi na kuhakikisha kutimiza ndoto walizojiwekea kwa maslahi mapata ya taifa.

Alisema mwakani watakongeza somo la hesabu kwenye zawadi ili kukamilisha kuwa na wanafunzi waliofanya vizuri katika masomo ya Kemia, Baiolojia, Fizikia na Hesabu. Kadhalika, alisema kuna wajibu wa serikali kuongeza uwekezaji kwa wanafunzi wanaomaliza masomo ya sayansi kusaidiwa kuanzisha gunduzi mpya ambazo baadaye zitazalisha faida.

Naye Mkemia Mkuu wa Serikali, Dk. Fidelice Mafumiko, alisema serikali imekuwa ikifanya jitihada za kufanya watoto wa kitanzania wanapata elimu bora.

"Jitihada hizo ni kutoa motisha kwa wanafunzi wanaofanya vizuri, kuwa na mifumo mizuri ya utoaji elimu, kuweka miundombinu rafiki kwa wanafunzi wote wanapata huduma bila kuangalia hali zao na sisi ofisi ya Mkemia tumeendeleza jitihada hizo kwa kutoa zawadi kwa wanafunzi wlaiofanya vizuri kwenye masomo yao," alisema.

Dk. Mafumiko alisema jitihada za GCLA za kuwapa zawadi wanaohitimu masomo ya sayansi kuanzia mwaka 2007 kwa kuanza ma masomo ya Kemia na jumla ya wanafunzi 384 na walimu 44 wamenufaika.

Alisema wako wanafunzi waliomaliza elimu na wapo wanaofanya kazi ndani na nje ya nchi akiwamo Mohamed Ally anayefanyakazi kampuni ya Facebook nchini Marekani.

Mmoja wa wanafunzi waliofanya vizuri kwenye somo la Kemia kutoka Shule ya Sekondari Arusha Day, Glory Mlagwa, aliishukuru ofisi ya Mkemia kwa kutoa motisha hiyo ambayo inawapa nguvu ya kusonga mbele katika kutimiza ndoto zao za kuwa wanasayansi.

# Watu wenye ulemavu waomba vifaa saidizi

**Na Enock Charles**

WATU wenye ulemavu wameiomba Serikali na wadau kuzingatia mahitaji ya vifaa saidizi na usaidizi wa kiuchumi katika sera mpya kwa watu wenye ulemavu.

Wamesema bado kuna uhitaji mkubwa kutokana na vifaa vinavyotolewa kutoendana na idadi iliyopo ya kundi hilo.

Katibu Mkuu wa Shirikisho la Watu Wenye Ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA), Jonas Lubago, akizungumza juzi katika maadhimisho ya Siku ya Teknolojia Saidizi Duniani jijini Dar es Salaam, alisema katika kundi hilo lenye zaidi ya watu milioni saba nchini, ni asilimia 11 tu hupata vifaa saidizi jambo linalowafanya kuwa tegemezi kiuchumi kwa ndugu zao na hivyo kutokutoa mchango wao wa kiuchumi kwa taifa.

"Wako watu wenye ulemavu ambao iwapo watapewa vifaa saizi kama vile fimbo nyeupe na viti mwendo, wanaweza kuendelea na shughuli zao za kiuchumi na kupunguza utegemezi kwa ndugu zao. Ni ombi langu kwa serikali na wadau kuzingatia kutoa vifaa saidizi kwa kundi hili.

"Serikali na jamii ziongeze jitihada hata ya kuwashawishi wazalishaji wa ndani wazalishe kwa wingi gharama zipungue lakini pia kuwa na vifaa vinavyoendana na mazingira yetu ya Kitanzania" alisema Lubago.

Mkurugenzi wa Kitengo cha Watu wenye Ulemavu , Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Rasheed Maftah, alisema tayari serikali imeshafanya tathmini ya hali halisi ya utekelezaji wa sera ya watu wenye ulemavu ya mwaka 2004 katika mikoa yote nchini na sasa timu ya wataalamu ipo katika hatua ya kuandaa tamko la sera mpya.

"Tayari serikali imefanya jitihada za kuboresha sera hii, tayari tumeshafanya tahmini ya utekelezaji wa sera ya mwaka 2004 kwenye mikoa yote ya Tanzania bara na ripoti imeshakamilika na sasa hivi timu ya wataalamu wanaenda sasa kwenye hatua ya kuandaa matamko ya sera iliyoboreshwa ya Huduma na Maendeleo kwa Watu Wenye Ulemavu" alisema Maftah.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la HelpAge Tanzania, Smart Daniel, alisema shirika hilo kwa muda mrefu limekuwa mtoa huduma mkuu wa teknolojia saidizi katika kambi za wakimbizi Kigoma na jamii zinazowazunguka kwa ufadhili wa serikali ya Ujerumani na shirika la Uingereza la Volant Charity ili kuboresha maisha ya watu wenye ulemavu.

Hata hivyo, alisema bado uhitaji ni mkubwa kwa vifaa saidizi kwa kundi hilo ikilinganishwa na mataifa yaliyoendelea ambako asilimia 90 ya wenye ulemavu hupata vifaa saidizi na kuomba serikali na wadau kutoa mchango wao katika kuwasaidia kupata vifaa saidizi ili kupunguza utegemezi na kuongeza uwezo wao wa kufanya kazi na kujitegemea kiuchumi.

Alisema kwa kushirikiana na Shirika la Afya Duniani (WHO) shirika limekuwa likiboresha upatikanaji wa vifaa saidizi kupitia miradi mbalimbali ikiwamo usambazaji wa vifaa saidizi 33,000 katika vituo 20 vya afya ya msingi nchini.

# Wakurugenzi waonywa fedha za walimu

**Na James Mwanamyoto,** KIGOMA

NAIBU Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) anayeshughulikia (Elimu), Dk. Charles Msonde, amewaonya wakurugenzi wa halmashauri nchini kuhusu fedha za uhamisho na likizo za walimu.

Amewataka wakurugenzi hao kuacha tabia ya kukopa fedha zinazopelekwa na serikali kuu kwa lengo hilo na kuzielekeza katika majukumu mengine, kitendo ambacho kinashusha ari na morali ya utendaji kazi wa walimu.

Dk. Msonde alisema hayo juzi kwa nyakati tofauti wakati wa vikao kazi vyake na maofisa elimu kata, wakuu wa shule, walimu wakuu na walimu katika Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma na Manispaa ya Kigoma Ujiji.

"Wakurugenzi wa halmashauri, ni marufuku kukopa fedha zinazoletwa na serikali kuu kwa ajili ya kulipa stahili za likizo na uhamisho wa walimu mnapozipokea. Zitumieni kulipa stahili hizo za walimu," alisema. Dk. Msonde alisema anazo taarifa za baadhi ya halmashauri kulalamikiwa kutolipa stahili za likizo na uhamisho wa walimu wa sekondari licha ya serikali kupeleka fedha katika halmashauri hizo ili ziwalipe walimu wanaodai.

"Nilimpigia simu ofisa elimu mmoja ambaye halmashauri yake inalalamikiwa na alikiri wazi kuwa serikali ilipeleka fedha lakini zilikopwa na kuelekezwa katika shughuli nyingine. Ofisa huyo aliniomba nimlinde ili asipatwe na tatizo kwa kutoa taarifa hiyo," alisema

Msonde aliongeza kuwa baada ya kupata taarifa hiyo, alizungumza na mkurugenzi husika ambaye alikiri halmashauri ilikopa fedha hizo, hivyo alimtaka mkurugenzi huyo kuwalipa walimu wenye madai na alitekeleza ndani ya siku tano.

Aidha, Dk. Msonde alihimiza kuwa suala la malipo ya stahili za likizo na uhamisho wa walimu ni maelekezo ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Mohamed Mchengerwa, ambaye amedhamiria kutatua kero zote za walimu ili wabaki na jukumu la kuunga mkono kwa vitendo jitihada za serikali za kuleta mapinduzi ya elimu nchini.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Kigoma, Josephat Kataga, alimshukuru Dkt. Msonde kwa ujio wake katika halmashauri hiyo na kumwahadi kuwa atasimamia utekelezaji wa maelekezo aliyoyatoa ili kutimiza azma ya kuboresha elimu inayotolewa nchini ili iwe na tija katika maendeleo ya taifa.

Dk. Msonde alihitimisha siku ya tatu ya ziara yake ya kuhimiza uwajibikaji mkoani Kigoma kwa kufanya vikao kazi na maofisa elimu kata, wakuu wa shule, walimu wakuu na walimu katika Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma na Manispaa ya Kigoma Ujiji.




Mkurugenzi wa Kitengo cha Watu wenye Ulemavu ,Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Rasheed Maftah akizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani) kuhusu masuala ya wenye ulemavu, kushoto ni Katibu Mkuu wa Shirikisho la Watu Wenye Ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA), Jonas Lubago na kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la HelpAge Tanzania, Smart Daniel **PICHA:ENOCK CHARLES**

# Kituo kupozea umeme kujengwa Bukombe

**Na Renatus Masuguliko,** GEITA

SERKALI, inatarajia kujenga kituo cha kupozea umeme Bukombe mkoani Geita kwa lengo la kuhakikisha wananchi wanapata huduma hiyo kwa uhakika ili waweze kujiletea maendeleo.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Dotto Biteko, alisema hayo jana wakati akiwahutubia wananchi wa Bukombe katika mkutano wa hadhara uliofanyika katika kata ya Igulwa.

Dk. Biteko alianza jana ziara ya siku tatu jimboni kwa lengo la kusikilza kero za wananchi na kuwafahamisha mipango na matarajio ya serikali kwa kile inachokitekeleza na kinachotarajiwa kutekelezwa kwa wananchi.

"Kujengwa kwa kituo cha kupozea umeme wilayani Bukombe, kutaondoa adha ya utegemezi wa kituo cha kupozea umeme cha Nyakanazi, kilichoko wilaya ya Biharamulo mkoani Kagera. Miundombinu hii itaongeza tija katika upatikanaji na usambazwaji ahuduma hiyo," alisema Biteko.

Alisema serkali inautambua mchango wa wananchi, hivyo kero zitakazotatuliwa katika jimbo hilo ni pamoja na ujenzi wa babarabara ya kutoka mamlaka ya mji mdogo wa Katoro, wilayani Geita kwenda Ushirombo itajengwa kwa kiwango cha lami, inatarajiwa kuchagiza kukuza shughuli za kiuchumi pindi itakapokamilika.

"Iko miradi mingine pamoja na kukamilishwa kwa ujenzi wa zahanati, vituo vya afya, shule za msingi na sekondari, ikiwamo kusudio la ujenzi wa kituo cha mabasi cha kisasa ni ushaihid tosha kuwa serkali inafanya kazi usiku na mchana kwa ajili ya kuwaletea maendeleo wananchi wake," alisema Biteko.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Geita, Martine Shigela, alisema mbali na serkali kuendelea kutatua kero za wananchi, hususani kuboresha na kujenga miundombinu ya barabara, afya,maji na huduma za kijami,ikiwemo kilimo na ufugaji,serikali itahakikisha kila wananchi wananufaika na rasilimali zilizopo hapa nchini,.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Geita, Nikolaus Kasendamila, akizungumza katika mkutano huo, alisema kuboreshwa kwa huduma za kijami ni uthibitisho tosha,kuwa serkali ya CCM itaendelea kusimamia na kuitekeleza Ilani yake kwa vitendo na siyo kwa maneno.

Mbunge wa Viti Maalum, Rose Busiga, aliseama katika mkutano huo, wananchi matamanio yao katika uchaguzi mkuu wa 2025 na wa serkali za mitaa wa 2024 ni kuipatia kura za kishindo CCM, ikiwa ni malipo ya ukarimu wanaotendewa na serkali.



## Uzalishaji vyakula mifugo waongezeka

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imesema uzalishaji wa vyakula vya mifugo vilivyosindikwa umeongezeka kutoka tani milioni 1.3 mwaka 2021/2022 hadi tani milioni 1.5 mwaka 2022/2023.

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, alisema hayo jana bungeni wakati akijibu sawali la Mbunge wa Viti Maalum, Jacqueline Msongozi (CCM), aliyetaka kujua serikali ina mpango gani wa kuboresha viwanda vya uzalishaji wa vyakula vya mifugo nchini.

Akijibu swali hilo Kigahe, alisema serikali imeendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji na kuhamasisha ujenzi wa viwanda nchini vikiwemo viwanda vya vyakula vya mifugo ambavyo vingi vinatumia malighafi za kilimo kama vile mahindi, soya na mashudu ya alizeti.

Alisema, kutoka na hali hiyo uzalishaji wa vyakula vya mifugo vilivyosindikwa umeongezeka kutoka tani 1,380,000 mwaka 2021/2022 hadi tani 1,580,000 mwaka 2022/2023.

Aidha, viwanda vipya 22 vya kuzalisha vyakula vya mifugo vimesajiliwa katika mikoa ya Arusha (vinne), Kilimanjaro (vitatu), Dar es Salaam (vinne), Morogoro (viwili), Iringa (vitetu), Mbeya (kimoja), Pwani (vitatu) na Shinyanga (viwili 2), hivyo kufanya viwanda vya kuzalisha vyakula vya mifugo kuongezeka kutoka 199 mwaka 2021/22 hadi 221 mwaka 2022/23.

Hata hivyo, alisema serikali itaendelea kuhamasisha uwekezaji katika viwanda vya uzalishaji wa vyakula vya mifugo na kuhakikisha kuwa vyakula vinavyozalishwa vinakuwa na viwango stahiki kulingana na mahitaji ya mifugo husika.

Katika swali nyongeza, mbunge huyo alitaka kujua mkakati wa serikali kupunguza kodi na tozo za vyakula vya mifugo vinavyotoka nje ili kuondoa mzigo wa bei kwa wananchi.

Kigahe alisema hivi sasa asilimia 60 ya vyakula vya mifugo vinavyotumika nchini vinaagizwa kutoka nje, hivyo mkakati wa serikali kwa sasa ni kuhamasisha uzalihaji wa ndani kwa kuanzisha viwanda ili kuwaondolea mzigo wa bei ya bidhaa hiyo wananchi.

# Wapewa vyeti kutambua mchango wao

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Singida (SUWASA) imetoa vyeti kwa wananchi, kanisa na serikali ya kijiji cha Manga kwa kutambua na kuthamini mchango wao.

Watu na taasisi hizo wamepewa vyeti hivyo kutokana na kutoa maeneo yao kwa ajili ya kupisha ujenzi wa mradi wa mabwawa ya kutibu majitaka unaojengwa katika Manispaa ya Singida kwa gharama ya Sh. bilioni 1.7.

Vyeti hivyo vilitolewa jana na Diwani wa Mtipa, Ramadhan Yusuph, baada ya maofisa wa SUWASA kufika katika eneo la Manga linalojengwa mradi huo kwa lengo la kutoa elimu kuwaeleza maendeleo ya mradi huo tangu ulipoanza kujengwa Mei, mwaka jana, hadi sasa.

Akizungumza baada ya kukabidhi vyeti, Yusuph aliwataka wakazi wa kata hiyo kuendelea kupokea na kufurahia miradi maendeleo inayotekelezwa ili kata ya Mtipa iweze kuendelea kwa haraka zaidi.

Naye Mhandisi Mazingira wa SUWASA, Richard Kasase, alisema ujenzi wa mradi huo umefikia asilimia 54 ya utekelezaji wake na shughuli mbalimbali za utekelezaji zinaendelea na unatarajia kukamilika Novemba 2024.

Kasase alieema kukamilika kwa mradi huu kutaboresha hali ya usafi wa mazingira katika Manispaa ya Singida na kuondoa umwagaji holela wa majitaka. Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa SUWASA, Hosea Maghimbi, aliwashukuru wananchi na Serikali ya kijiji cha Manga kwa kutoa ushirikiano katika utekelezaji wa mradi huu tangu ulipoanza Machi, mwaka huu, Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, alipotembelea mradi huo, aliiagiza SUWASA kusimaia mradi wa ujenzi wa mabwawa ya kutibu majitaka uili ujenga vizuri na uweze kulingana na thamani ya fedha.

Naye Meneja wa SUWASA, Sebastiani Warioba, alimweleza mkuu wa mkoa kuwa kujengwa kwa mradi huu ni ukombozi mkubwa kwa Manispaa ya Singida kwa kuwa kwa kipindi kirefu majitaka yalikuwa yakitupwa porini jambo ambalo kiafya sio zuri

"Faida ya mradi huu kwa wananchi utawawezesha kupata huduma ya usafi wa mazingira kwa kuondoa majitaka kwenye makazi yao na kuongeza shuguli za maendeleo ikiwemo kuendesha kilimo cha mboga mboga," alisema. Warioba alisema Singida imebahatika kuwekwa katika mpango wa mradi wa miji kumi ambao utawezesha kujengwa kwa mtandao wa majitaka kwa kujengwa kutoka kwenye makazi.



Wabunge wa Mkoa wa Singida, Musa Sima wa Singida Mjini (kulia), Ramadhani Ighondo wa Singida Kaskazini (kushoto) na Miraji Mtaturu wa Singida Mashariki, wakijadiliana jambo, nje ya ukumbi wa Bunge, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Waziri afafanua tofauti kodi pango na jengo

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

NAIBU WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geofrey Pinda, ametoa ufafanuzi juu ya mkanganyiko ambao umekuwa ukijitokeza kwa wananchi juu ya tofauti iliyoko kati ya kodi ya pango la ardhi na kodi ya majengo.

Pinda alitoa ufafanuzi huo jijini hapa juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mkanganyiko huo wa kati ya kodi ya pango la ardhi maana yake, utaratibu na njia ya ulipaji.

Alisema kodi ya pango la ardhi kama ilivyoekekezwa hutozwa ni kwa wamiliki wa ardhi, tofauti na kodi ya majengo ambayo hutozwa kwenye majengo au nyumba.

Alisema kodi ya majengo imewekewa utaratibu wa ulipaji na ukusanyaji wake ambapo kwa sasa inalipwa kwa njia ya malipo ya ununuaji wa umeme kupitia mfumo wa luku.

"Hapa ninataka kusisitiza kwa wamiliki wote wa ardhi hapa nchini, kutekeleza sharti la kulipa kodi ya ardhi kwa kuwa sasa tumeboresha njia za ukadiriaji na ulipaji wa kodi husika kwa njia ya kidigitali," alisema.

Pinda pia alikumbusha maelekezo yaliyotolewa na Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi wakati wa kuhitimisha hotuba ya bajeti mwaka 2024 Bungeni.

Alisema wizara hiyo imedhamiria kuchukua hatua kwa wamiliki wote wa ardhi watakaoshindwa kutimiza masharti ikiwemo kuwafikisha mahakamani ili kuuza mali zao kufidia kodi ya ardhi na kupendekeza ubatilisho wa milki zao.

Katika hatua nyingine, Pinda alisema malipo ya kodi ya pango la ardhi hufanyika kwa kuzingatia ukubwa wa ardhi inayomilikishwa na matumizi yaliyoidhinishwa na thamani yake na kiwango cha malipo.

Pia alisisitiza kuwa ardhi yote ya Tanzania ni ya umma, hivyo raia yoyote wa Tanzania anayo haki ya kuishi na kutumia kwa mujibu wa sera na sheria za ardhi.

Alisema kuwa haki hiyo inatoa masharti mbalimbali kwa wamiliki wa ardhi miongoni mwake ikiwa ni la kulipa kodi ya pango.

Alisema haki nyingine ni malipo ya kodi inayotozwa kwa wamiliki wa ardhi kutokana na fursa wanayopata ya kupangishwa ambayo ni ya umma.





# Kasi maambukizi malaria yazidi kupaa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIKA kipindi cha Julai, mwaka jana, hadi Machi, mwaka huu, ugonjwa wa malaria umeongezeka kwa kiasi kikubwa visiwani Zanzibar ikilinganishwa na mwaka 2022/23 huku sababu kubwa ikitajwa kuwa mabadiliko ya tabianchi.

Sababu nyingine inaelezwa kuwa kuongezeka kwa wagonjwa wa malaria kunatokana na jamii kutokuuchukulia umakini ugonjwa huo hali ambayo imesababisha kuchelewa kufika katika vituo vya afya. Akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Afya kwa mwaka 2024/25, Waziri wa Wizara hiyo, Nassor Ahmed Mazrui, alisema kwa mwaka 2023/24 washukiwa 442,939, wakiwamo 392,042 kutoka Unguja na Pemba 50,897, wamechunguzwa vimelea vya malaria na 19,579 (wanaume 14,569 na wanawake 5,010) sawa na asilimia 4.42, waligundulika kuwa na vimelea hivyo.

Mazrui alisema hali hiyo imeonyesha ongezeko kubwa ikilinganishwa na mwaka 2022/23 ambapo washukiwa wa malaria 235,862, Unguja 205,553 na Pemba 30,309 na waliogunduliwa na vimelea vya malaria ni 2,194 ambao kutoka Unguja walikuwa 1,992 na Pemba 202.

"Katika miaka yote miwili maambukizi yameonyesha kuwa makubwa sana kwa upande wa Unguja ikilinganishwa na Pemba," alisema.

Waziri Mazrui pia alisema wagonjwa 1,593 walipata malaria kali na kulazwa katika hospitali mbalimbali za Unguja na Pemba huku vifo 29 vikiripotiwa kutokana na malaria. Mazrui alisema asilimia 82 ya maambukizi yaliyoripotiwa yanatoka mkoa wa Mjini Magharibi na wilaya iliyotoa wagonjwa wengi ni Mjini Unguja kwa asilimia 52.9 ikifuatiwa na Magharibi B asilimia 20.3. Alisema takwimu zimeonyesha kuwa waathirika wakubwa ni wanaume wenye umri kati ya miaka 15 na 45 kwenye makundi ya wanafunzi, walinzi, wajenzi, watembeza watalii, wenye bodaboda na baba lishe. "Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea kupiga dawa katika maeneo yanayotoa wagonjwa wa ndani wa malaria katika Wilaya zote 11 na kutoa elimu juu ya kinga na kumaliza ugonjwa wa malaria," alisema. Waziri huyo alisema nyumba 11,047 zikiwamo 8,025 Unguja na Pemba 3,022 kati ya nyumba 11,154 sawa na asilimia 99 zilipigwa dawa ya kuua mbu wa malaria na vyandarua 93,225 vilitolewa vikiwamo Unguja 62,265 na Pemba 30,960 kwa wajawazito na watoto chini ya mwaka mmoja kupitia vituo vya afya.

Hata hivyo, alisema jumla ya vyandarua 252,155 viligawiwa kwa jamii katika shehia 75 za mkoa wa Mjini Magharibi kwa ajili ya kinga ya malaria.

"Naomba kuchukua fursa hii kuwaambia wananchi na taasisi husika kuwa malaria bado ipo, hivyo jamii inapaswa kuchukua tahadhari katika maeneo ili kujikinga na ugonjwa huu kama kaulimbiu inavyosema 'Nipo Tayari Kuishinda Malaria! Ziro Malaria Inaanza na Mimi,'" alisema Mazrui.



Baadhi ya wageni wakifuatilia hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, iliyowasilishwa katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani nje kidogo ya Mji wa Zanzibar juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Uwekezaji hoteli kitalii washika kasi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Utalii na Mambo ya Kale, Mudrik Ramadhan Soraga, amesema miradi ya uwekezaji katika hoteli visiwani Zanzibar imefikia 260 na asilimia 70 iko katika ujenzi wa hoteli za hadhi ya nyota tano.

Amesema uwekezaji wa hoteli hizo una maana kubwa katika jamii na taifa kwa sababu unachochea ukuaji wa uchumi na ustawi wa jamii.

Soraga aliyasema hayo jana visiwani hapa wakati akizindua mradi wa ujenzi wa hoteli yenye hadhi ya nyota tano huko Michamvi, Kusini Unguja.

Alisema uwekezaji wowote wa utalii lazima ufuate sera ya utalii endelevu wa utalii wa kijani ili kulinda na kuhifadhi mazingira.

Kwa mujibu wa Soraga, lazima suala la mazingira lizingatiwe katika uwekezaji hasa ikizingatiwa kuwa Zanzibar ni kisiwa, hivyo bila ya uwapo wa uhifadhi wa mazingira ikiwamo upandaji wa miti, kisiwa kitaangamia.

Alisema visiwa vya Zanzibar vina ushindani mkubwa hasa katika sekta ya utalii na kwamba Zanzibar inashindana na visiwa mbalimbali duniani, hivyo inahitaji wawekezaji wengi na wenye uwezo mkubwa zaidi.

Naye mwekezaji wa mradi huo, Simon Nikitas, alisema mradi utakapokamilika unatarajiwa kugharimu dola za Marekani milioni 10 na utajumuisha majengo ya kifahari mengine yakiwa katika fukwe na ndani ya maji ya bahari katika eneo hilo.

Alisema wamehamasika kuwekeza Zanzibar kutokana na mandhari mazuri lakini pia hali ya amani na utulivu uliopo ambao unawavutia wageni wengi zaidi kutembelea visiwa hivyo.

Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ayoub Mohammed Mahmoud, alisema ndoto ya mkoa huo ni kuhakikisha kasi ya ukuaji wa maendeleo unaimarika kwa kiwango kikubwa ili wananchi kupata maendeleo.

Ayoub alisema lazima wananchi kwa kushirikiana na wawekezaji kushiriki katika shughuli za upandaji wa miti ili kulinda na kuhifadhi mazingira na kuendeleza utalii. end

# Othman ahimiza umakini matumizi maliasili

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, ameitaka jamii kuzitumia kwa ungalifu maliasili zilizopo kwa kufuata miongozo, sheria na taratibu kwa kuwa mazingira ndio uhai wa mwanadamu.

Othman aliyasema hayo juzi katika viwanja vya Mshaame Mata, Micheweni mkoa wa Kaskazini Pemba, alipozungumza katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani.

Alisema wananchi kwenda kinyume cha miongozo hiyo kunaweza kuisababishia Zanzibar madhara makubwa yanayotokana na janga la kimazingira kutokana na kuendelea kwa kasi ya mabadiliko ya tabianchi.

Makamu huyo alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar licha ya kuchukua juhudi za kunusuru mazingira kwa kupanda miti ya misitu, baadhi ya wananchi hawajaona umuhimu wa kupanda miti na wanaendelea kuikata iliyopandwa na kutunzwa tokea asili, alisema hali hiyo inaweza kusababisha madhara zaidi ya kimazingira nchini na kuathiri ustawi na uhai wa binadamu.

Othman alisema kufanya hivyo ni dhahiri kwamba kunachangia kuendelea kupotea uoto wa asili na kwamba hata matunda ya asili sasa ni adimu kuonekana sambamba na miti ya misitu na matunda, baianuai kupotea, hivyo kuongezeka kwa athari za mabadiliko ya tabianchi.

Alitoa wito kwa jamii kupanda na kuitunza miti sambamba na misitu iliyopo pamoja na baianuai zake ili kuimarisha mazingira kwa manufaa ya taifa na kizazi cha sasa na kijacho. Ili kukabiliana na hali hiyuo, alisema ni vyema kila mwananchi kujiwekea lengo la kupanda miti angalau mitatu kwa mwaka.

Alisema jitihada za upandaji miti kwa sehemu stahiki zinahitaji kuelekezwa kwa miti ya matunda na kwamba kufanya hivyo pia ni sehemu ya ibada ambayo ni sadaka endelevu ambayo ina manufaa makubwa ya kidunia na akhera.

Othman alisema katika kuendeleza juhudi za utunzaji wa mazingira Zanzibar, ofisi yake imeandaa mpango maalum wa kuirithisha Zanzibar kuwa ya kijani na kuwataka wananchi kutoa ushirikiano mkubwa wakati wa utekelezaji wa mradi huo utakapowadia kwa kuwa ni mkombozi dhidi ya mabadiliko ya tabianchi.

Pia alisema hivi sasa kina cha maji ya bahari kimepanda kutokana na ukataji mkubwa wa miti ya mikoko jambo linalochangiwa na mabadiliko ya taibianchi na vitendo vya wanadamu, hivyo kuwapo uharibifu wa mazingira.

Othman aliitahadharisha jamii kuepuka matumizi makubwa ya dawa na kemikali za kusafishia vyoo ambazo pia zina athari kubwa katika afya ya udongo jambo ambalo linachangia kuwepo uharibifu mkubwa wa mazingira.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Harous Said Suleima, aliwataka wananchi kuacha kuharibu wa mazingira na kufanya hivyo ndiko kuinusuru Zanzibar na vizazi vijavy.

Aliwataka wananchi kuendeleza juhudi za upandaji miti katika maeneo yao ya kuishi kwa kutumia wataalamu waliopo ili kuweza kupata ushauri sahahi wa kila mmoja ndani ya nyumba ya kuishi kuwa na mti alioupanda na kuutunza.

Naye Mkuu wa wilaya ya Micheweni, Mgeni Khatib Yahya, alisema mkoa huo hasa wilaya ya Micheweni, inaendelea na mkakati mkubwa wa upandaji miti ya aina mbalimbali ikiwa ni juhudi za kuunga mkono serikali katika kuhifadhi mazingira.



**ROMA**
UKURASA 13

Nipashe
MWANGA WA JAMII

BT
BURUDANI TELE

JUMAMOSI JUNI 8, 2024



# TAJIRI WA SAUTI

## ANAYETAFUTA NJIA ALIYOTOKEA

MIAKA 10 iliyopita jina la Rich Mavoko, lilikuwa likitawala katika midomo ya wapenda muziki wa Bongo Fleva Afrika Mashariki.

Katika vibao pendwa vya msanii huyo kama vile Pacha Wangu na Roho Yangu ilikuwa ni vugumu watu kuacha kujitikisa kutokana na mapigo yenye ushawishi na sauti tamu kutoka kwa tajiri huyo wa sauti.

Kwa sasa Rich Mavoko, anajitahidi kujifufua kwa kutoa nyimbo mbalimbali, lakini bado hajaweza kuliteka soko na badala yake bado kiza kinazidi kumwandama.

Katika kibao chake kipya alichokitoa My G, ameonekana kutoka katika aina yake ya uimbaji na kutumia mtindo wa kughani ambao umeonekana kuwa tofauti sana.

Baadhi ya wadau wa muziki wamesema, kupotea kwa Rich Mavoko kulianzia pale alipoacha utawala wake na kuamua kujiunga na WCB na kujikuta akipoteza mwelekeo.

kwa kutumia sauti laini yenye hisia, na kwenda katika kughanimwezi huu, kisa amesema alishtushwa na taarifa zilizokuwa zinasambaa mtandaoni kuwa ameomba msamaha ili arudi kufanya kazi na WCB Wasafi.

"Ukimsikiliza Rich Mavoko wa sasa sio yule wa miaka kumi iliyopita, amejaribu kuridi lakini ameathiriwa na aina ya miziki aliyokutana nayo alipokuwa amejiunga na WCB mwaka 2018," amesema Christopher Mjana.

Amsema kama uwezo wa kurudisha umaarufu wake bado anao, lakini anatakiwa kutambua kwa nini amefika hapo na nini anatakiwa kufanya ili kuwa kama nyuma.|

"Watu walimpenda kwa sauti yake, walipenda mashairi yake, hilo ndilo anatakiwa kujua na kulifanyia kazi haraka kabla ya umri hajamtupa," ameongeza.

BASI SAWA

## Shamsa amfagilia mume wake



MWIGIZAJI wa filamu za Bongo muvi, Shamsa Ford, ameamua kuweka hisia zake kwa mume wake Mililo na kumuelezea kama mtu anayempa Amani katika maisha.

Katika ujumbe wake kwenye ukurasa wa Instagram, Shamsa, amemtaja mume wake kama mtu mwenye upendo na kuwa baba bora ndani ya familia yake.

"Tumepitia mengi makubwa ya kukatisha tamaa lakini upendo ndio ulizidi kuwa mkubwa kati yetu.. Nakushukuru sana kwa kunipenda na kuniheshimu ,nakushukuru sana kwa kusimama baba bora kwenye familia yetu..Siku zote za maisha yako tambua una mke bora mwenye kukupenda kwa dhati," ameandika.

## Acheni kumkera Zari



MREMBO Zari Hassan, amewajia juu watu wanaotabiri mwisho wa ndoa yake na mumewe, Shakib Lutaaya, akisema kile wanachokiomba kamwe hakitatokea.Akizungumza na mashabiki wake kupitia Instagram, Zari amesema kuna wanaomuhukumu kwamba kutokana na kuishi na wanaume tofauti, hivyo hawezi kudumu na mwanume huyo ambaye ni mdogo kwake.

"Wanadai nimelala na wanaume wengi, lakini siwezi kutoa ushahidi. Watu hubadilika wanapokutana na mtu. Hawafanyi tena walivyokuwa wakifanya zamani," amesema Zari.



## ESTHER USIENDE MBALI, WENGI WAPO NA WEWE

MWIGIZAJI maarufu kutoka Kenya, Esther Chebet, amewaweka katika hali ya hofu mashabiki zake kutokana na kutuma machapisho yenye ujumbe wa kukata tamaa juu ya maisha yake.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, msanii huyo wa filamu aliandika hali anayojisikia kuhusu maisha yake na kusababisha idadi kubwa ya watu kutaka aangaliwe kwa umakini hasa kutokana na kujulikana ana matatizo ya afya ya akili.

"Sijui kama mwisho wa siku nitakuwa sawa, lakini nilijiingiza kwenye kitu ambacho siwezi kukibadilisha kabisa. Maisha ni ya kiroho na nadhani nilijiingiza katika ulimwengu mbaya katika kutafuta amani, akili na kuguswa na nguvu mbaya," moja ya jumbe zake ilielezea.

## FILAMU

## Kaburi la maombi balaa

**Na Adam Fungamwango**

"KABURI la Maombi." Ndivyo jina la filamu hiyo linavyoitwa. Imechezwa na Sharifu Kumwenda, aliyecheza kama Derrick, Blandina Dastan, akiekti kama Kalunde, Mohamed Fungafunga, yeye ni Chifu Kumwenda, Ally Luanda akacheza kama David.

Filamu hii inaonyesha jinsi baadhi ya Waafrika wanapoelimika, yaani kusoma, wanaweka kando asili na utamaduni wao.

Kila kitu kwake anakiona cha kishamba na kilichopitwa na wakati. Wana tabia ya kuviona vitu vya kizungu kuwa ni bora, mali, vya kisasa, visivyokuwa na matatizo yoyote.

Inaanza kuonyesha kuwa David anarejea kijijini kwao, baada ya miaka mingi kuishi mjini, kusoma na kupata kazi. Anarejea akiwa na rafiki yake aliyempata huko huko mjini anaitwa Derrick.

Ile kufika tu kwanza kila kitu cha huko alikiona ni kichafu, na hakifai. Aliwatimua mpaka akinadada waliokuwa wanakwenda kumsalimia.

Jamaa akalikana hadi jina lake la asili Mulangala. Akakataa hata baba yake asimwite hilo jina, bali David tu.


Siku chache zikabaki kabla ya wanakijiji kwenda kutambika kwenye kaburi na aliyekuwa chifu wao, Kumwenda. David yeye akakataa, akasema hawezi kufanya kitu kama hicho kwa sababu ni msomi.

David alianza kumpenda msichana mmoja kijijini aitwaye Kalunde, lakini kutokana na nyodo zake, akakataliwa. badala yake Derrick ndiyo akachukua nafasi hiyo kwani pamoja na kwamba ni mgeni, alizoeana na watu wote, alikuwa mkarimu, kiasi cha kupendwa na wanakijiji.

Uhusiano wa Derrick na Kalunde ulimkera David, akakorofishana na rafiki yake.

Baba yake akafariki dunia, na mama yake akawa mgonjwa. David hakujali ugonjwa wa mama yake akaamua kurudi Dar es Salaam. Derrick aligoma kutokana na hali ya mama wa rafiki yake.

Siku ya tambiko ilifika, Derrick naye alikaribishwa. Kufika kwenye kaburi, mzimu ukatokea na kubainisha kuwa mgeni huyo ndiye atakuwa mtawala wa himaya hiyo, kwa sababu ni mtoto wa Chifu huyo aliyezaa na mwanamke mmoja ambaye aliondoka na ujauzito wake, miaka mingi iliyopita.








## Roma mpeni maua yake

RAPA mwenye mashairi yenye utata, Roma Mkatoliki, amesema albamu yake mpya aliyoitambulisha juzi 'Nipeni Maua yangu' ni tiba maalum kwa watu wenye shida za kimaisha.

Roma ambaye kwa sasa anaishi Marekani, amesema kwamba albam hiyo ambayo inapatikana katika majukwaa ya kidijitali ya kuuza na kusambaza muziki, ina ujumbe wa kuwapa ujasiri vijana kusaka maisha licha ya kupitia changamoto mbalimbali.

"Ni albam maalumu kwa wale wote wanaopitia changamoto za kimaisha na wamekata tamaa ya maisha wanahisi kuanguka na wanataka kusimama tena," amesema Roma.

## MAKUKA YEE, BADO GITA LAKO LIPO

**Na Adam Fungamwango**

MAKUMBELE ni wimbo maarufu sana nchini ambao ulipigwa na bendi ya Maquiz Original. Ulikuwa ni utunzi wake hayati Kaumba Kalemba mwanzoni mwa miaka ya 1990.

Mmoja wa walioshiriki kwenye wimbo huo, akipiga gitaa la rythm, Omari Makuka, amefariki dunia.

Makuka alifariki dunia Juni 8, 2021, Dar es Salaam. Mwanamuziki huyo aliyekuwa akiishi Mtaa wa Aggrey, Kariakoo, alizikwa Juni 9 kwenye Makaburi ya Kisutu, Dar es Salaam, msiba ukiwa ulikuwa kwa mtoto wake Ukonga Sitakishari.

Mwanamuziki huyo, atakumbukwa kutokana na mchango wake mkubwa kwenye tasnia ya muziki, akihudumu bendi mbalimbali kama Super Matimila, Maquiz Original, UDA Jazz na MK Group.

Mwanamuziki huyo alikuwa na uwezo mkubwa wa kupiga gitaa la solo,  la kati Pamoja na rhythm.

Kwenye safu hii tutaangalia baadhi ya nyimbo maarufu ambazo ameshiriki.

### Natoa Onyo-Super Matimila

Ni wimbo ambao ulitungwa na Dk. Remmy Ongala mwanzoni mwa miaka ya 1980 ambao unawaonya wale kwenye tabia ya kupenda wake na waume za watu. Wanaambiwa kuwa mke wa mwenzio usimvalie koti, wala mume wa mwenzio usipakalie wanja. wenye tabia hiyo wanaonywa, mkuki mtamu kwa nguruwe, kwa binadamu mchungu. Makuka alipiga rhythm kwenye wimbo huo.

### Alimasi-Super Matimila

Kwenye wimbo huu pia marehemu, Makuka alipiga gitaa la kati, rhythm. Ulikuwa utunzi wake marehemu Kasaloo Kyanga mwanzoni mwa miaka ya 1980 na ukiusikiliza wimbo huu kuna sehemu mtunzi alinogewa na wimbo na kupiga kelele 'Makuka Yee'. Ni wimbo unamhusu mwanamke anayemlalamikia mume aliyemtelekeza na watoto na kusababisha kuishi kwa tabu.

### Sakina-Uda Jazz Band

Huu ni utunzi wake mwenyewe Omari Makuka na yeye mwenyewe kupiga gitaa la solo. Hapa alikuwa kwenye bendi ya Uda Jazz akiwa kama kiongozi wa bendi.

Ni wimbo unaomzungumzia binti mmoja denti Sakina ambaye badala ya kwenda shule anakwenda kufanya starehe. Anatoka na nguo za shule, akifika huko anabadilisha, shati la shule anatia kwenye mkoba wa shule na kuvaa la ndege. Ni mashati ambayo katikati ya miaka ya 1980 yalikuwa maarufu sana na yalivaliwa na wajanja na watoto wa mjini tu.

### Makumbele-Maquiz Original

Mwanzoni mwa miaka ya 1990, Maquiz Original ilitoa kibao kilichotokea kupendwa sana, 'Makumbele'. Ni utunzi wake marehemu Kaumba Kalemba. Hayati Makuka alikuwa ameshalipa kisogo kundi la Uda Jazz na kuhamia bendi hii. Kwenye wimbo huu alipiga second solo au mini solo, gitaa ongozi la solo likipigwa na Dekula Vumbi Kahanga.


Ni wimbo ambao mwanamke amevumilia mengi kutoka kwa mumewe, lakini sasa ameshinda na kufika mwisho.



### Maumivu Makali-MK Group

Ni wimbo mkali sana ambao ulitungwa pia mwanzoni mwa miaka ya 1990, Makuka akiwa amejiunga sasa na bendi ya MK Group 'ngoma za maghorofani,' wakati huo wakipiga New Africa ghorofa ya saba.

Wimbo huu ulitungwa na aliyepiga solo kwenye wimbo huo, marehemu Joseph Mulenga, marehemu Makuka akipiga rhythm.



# Kanye kayakanyaga tena

RAPA maarufu wa Marekani, Kanye West, anazidi kukabiliwa na matatizo ya kisheria baada ya mwanamke mmoja kumfungulia mashtaka akidai kumnyanyasa kingono.

Pisciotta, ambaye alikuwa mfanya kazi wa West kwa miaka miwili, amedai alimtumia ujumbe wa ngono na kumfanyia vitendo visivyofa wakati wa uongozi wake.

Hata hivyo, West bado hajajitokeza hadharani kujibu tuhuma hizo.

Kulingana na jalada hilo, lililopatikana na The Blast, Pisciotta aambaye ana uzoefu wa miaka 15 katika tasnia ya muziki. West alimwajiri kama mshiriki mbunifu kwenye kampuni yake ya mitindo ya wanawake ya Yeezy Season, mnamo 2015.



## Mahabusu Uganda tatizo kwa Tems

MWANAMUZIKi kutoka Nigeria, Nasboi ameweka wazi kwamba hahitaji ruhusa kutoka kwa wazazi wake kuoa mwanamke anayempenda.

Katika mazungumzo yake hivi karibuni, mwimbaji huyo alieleza kwa nini anaweza kufunga ndoa na mwanamke hata kama mama yake hajamkubali.

Amesema katika historia ya familia yake haina tatizo la ukabila na anaweza kukutana na kupanga ndoa na mwanamke anayempenda bila kupata ruhusa ya wazazi.

## Seun anayatamani matunda

MWANAMUZIKI kutoka Nigeria Seun Kuti, ameijia juu Serikali kutokana na kufumbia macho upandaji wa miti ya matunda katika jiji la Lagos.

Hivi karibuni Seun Kuti, amekuwa akiishambulia serikali katika masuala mbalimbali.

Msanii huyo wa muziki wa Afrobeats, amesema zamani kulikuwa na aina nyingi za miti ya matunda imetanda katika mji huo, lakini yote imekatwa au kuharibiwa,

"Kuna watu wenye njaa kwa nini serikali isipande miti Lagos yote? Hakuna kitu haya miti ya matunda imepotea tunahitaji serikali kusaidia kuipanda," amesema.





## Oprah amkumbuka kaka yake

MTANGAZAJI maarufu wa vipindi vya maisha, Oprah Winfrey, amefanya maadhimisho ya kumkumbuka marehemu kaka yake, Jeffrey Lee, ambaye alifariki miaka 35 iliyopita kwa ugonjwa wa Ukimwi.

Katika video iliyosambaa mtandaoni, Oprah alifichua kuwa Jeffrey aliaga dunia akiwa na umri wa miaka 29 tu mwaka 1989, wakati ambao alielezea kama ulikuwa wa ukatili kwake.


Oprah amewaambia watu waliohudhuria katika kumbukumbu hiyo kuwa kama angekuwa hai kaka yake, mambo mengi yangebadilika.

## Thuso ndani ya The Lion King

MSANII filamu kutoka Afrika Kusini, Thuso Mdebu amejiunga rasmi katika uigizaji wa kazi mpya ya Mufasa, inayoitwa The Lion King akiwa na mchekeshaji mkongwe Kagiso Lediga.

Thuso anaungana na waigizaji nyota wa filamu hiyo maarufu ndani ya Afrka Kusini, inayotarajiwa kuonyeshwa kwa mara ya kwanza Desemba mwaka huu.

Kujiunga kwa msanii huyo katika filamu hiyo ni kutokana na umahiri wake wa kuigiza na mara nyingi anapofanya kazi huwa anaacha gumzo kutoka kwa watazamaji.







# Vijana 64 wanaswa kwa tuhuma uhalifu

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

VIJANA 64 kutoka mikoa mbalimbali nchini, wamekamatwa na Jeshi la Polisi mkoa wa Tanga kwa tuhuma za kujihusisha na uhalifu wa biashara isiyo halali ya kimtandao, ambayo inajulikana kama Q-net.

Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Balozi, Dk. Batilda Buriani, alisema vijana hao wamekuwa wakiwapigia simu wazazi na kuwataka kutoa fedha ili vijana wao waweze kupata ajira kupitia bidhaa zao wanazouza. Dk. Buriani alifafanua kuwa vijana hao wakiwemo wavulana 29 na wasichana 35, viongozi wao wapo jijini Dar es salaam wakati mikoani wakiwatuma wao kufanya kazi hiyo.

"Tumeona vijana ambao ndiyo nguvu kazi ya taifa, kuanzia miaka 19 hadi 24 na wengine wamefika hadi vyuo vikuu, lakini hakuna wanachofanya, kazi ni hiyo ya utapeli," alisema.

Aidha, Dk. Buriani alitoa rai kwa wazazi kuwa makini endapo kama watapigiwa simu na watu wasiowajua wakidai kutoa nafasi za ajira hasa za kimtandao.

"Huu utaratibu wa wazazi mnapigiwa simu kuna nafasi za kazi na ninyi mnawaruhusu wanakwenda, huu ni utapeli mtupu tuweni makini hasa na mitandao," alibainisha.

Mkuu huyo alisema vijana wote waliokamatwa watasaidiwa kupatiwa mafunzo katika vyuo vya veta ili kuweza kupata elimu ya ujasiriamali itakayowasaidia kupata ujuzi katika maeneo yao.

"Tanga ni Mkoa salama na hakuna nafasi ya kufanya biashara ambazo hazitambuliki, lakini pia vijana hawa watarudishwa katika maeneo yao chini ya uangalizi maalumu,"alisisitiza.

# Wabuge wa Marekani watua kujifunza uhifadhi

**Na Godfrey Mushi,** NGORONGORO

WABUNGE wa Bunge la Congress la Marekani, wametua nchini kujifunza na kupata uzoefu wa shughuli za uhifadhi na namna unavyochangia kuvutia watalii wengi wa kimataifa.

Pamoja na mambo mengine, wanataka kuona jinsi sera za uhifadhi za Marekani, zinavyoweza kuchangia athari chanya kwa uhifadhi na utalii wa bara la Afrika.

Jana, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge la Congress inayoshughulikia Maliasili, ambaye ni Mbunge wa Arkansas, Bruce Westernman, alisema yeye na wenzake wamefanya uamuzi wa kuitembelea Tanzania, ikiwamo Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA).

Westernman alisema wamefurahishwa kuona namna uhifadhi endelevu ulivyoongeza idadi ya wanyamapori mbalimbali wanyamapori wakubwa watano ambao ni faru, simba, chui, tembo na nyati.

"Kamati yangu inaipongeza Tanzania kwa juhudi za uhifadhi zinazofanywa na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, husussan utunzaji na ulinzi wa wanyamapori adimu kama faru, wakiwa katika maeneo yao ya asili.

"Timu yetu tunafanya ziara hii kama sehemu ya mafunzo ya kuona juhudi za uhifadhi kwa nchi za Afrika. Tunaangalia ili kuona namna gani sera za Marekani, zinaweza kuwa na ushirikiano chanya kwenye sekta ya uhifadhi na utalii kwa Hifadhi za Bara la Afrika," alisema.

Akizungumza na ujumbe huo wa Bunge la Congress, Kamishna wa Uhifadhi wa NCAA, Dk. Elirehema Doriye alisema serikali ya Tanzania imeendelea kuhakikisha vivutio vya utalii vilivyoko Ngorongoro vinalindwa, kutunzwa na kuhifadhiwa.

Kwa mujibu wa Dk. Doriye, NCAA inafanya kazi kubwa ya kuibua mazao mapya ya utalii, kwa ajili ya kuvutia wageni wa mataifa mbalimbali wanaotembelea eneo hilo kwa shughuli za utalii, utafiti na elimu ya masuala ya uhifadhi wa rasilimali za wanyamapori na utunzaji wa mazingira.

Awali, Naibu Kamishna wa Uhifadhi (Uhifadhi, Utalii na Maendeleo ya Jamii), Victoria Shayo, aliueleza ujumbe huo kuwa pamoja na juhudi za uhifadhi katika eneo la Ngorongoro, kumeliwezesha eneo hilo kupata hadhi tatu za kimataifa zinazotambuliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO).

Alizitaja hadhi hizo kuwa ni tabaka hai la kimataifa, urithi mchanganyiko wenye historia ya binadamu katika eneo la Olduvai na Laetoli na eneo lenye sifa ya utalii wa miamba na jiolojia (Ngorongoro Lengai UNESCO Global Geopark).

Naye Ofisa Utalii Mkuu wa NCAA, Peter Makutian, alisema Ngorongoro ina vivutio vingi na vya kipekee duniani, ikiwemo wanyamapori wa aina mbalimbali, kreta za Ngorongoro, Olmoti, Empakai, makumbusho ya Olduvai na Marry Leakey.

Umo pia mchanga unaohama, tambarare za Ndutu na Mlima Olmoti ambao ni wa tatu kwa urefu Tanzania.



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, Dk. Jumaa Mhina (kushoto), akipata maelezo kutoka kwa Mjasiriamali wa Kikundi cha Mbomole Spices, Dastan Daffa (katikati), kuhusu namna ya kutumia bidhaa za mazao ya viungo, alipotembelea banda la halmashauri hiyo, katika Maonyesho ya Biashara na Utalii kwenye viwanja vya Shule ya Sekondari ya Usagara, jijini Tanga mapema wiki hii. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Askofu matatani kwa madai kuchoma makazi ya wananchi

**Na Hamida Kamchalla,** HANDENI

MKUU wa Wilaya ya Handeni mkoani Tanga, Albert Msando, ameagiza Jeshi la Polisi, kumtafuta na kumkamata kiongozi mkuu wa kanisa moja nchini, anayedaiwa kuzusha taharuki wilayani hapa baada ya kubomoa nyumba za watu bila taarifa.

Kiongozi huyo ambaye ni askofu, kwa sasa anasakwa na polisi ili kupelekwa Handeni, kwa amri ya mkuu wa wilaya.

Msando alitoa amri hiyo juzi alipokuwa katika kijiji cha Michungwani, kata ya Segera, baada ya wananchi kuwasilisha kwake malalamiko ya kuvunjiwa makazi yao. "Nimekuja hapa kuona hali halisi na agizo langu ni moja tu, OCD (Mkuu wa Polisi wa Wilaya) na OC CID (Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai Wilaya) huyo askofu (anamtaja jina) atafutwe na akamatwe yeye mwenyewe na si mwakilishi.

"Aje atoe maelezo yake kwa nini ametoa amri ya kuvuniwa kwa nyumba ya mtu mwenyewe akiwa ndani. Kama alikwenda mahakamani kufungua hati ya dharura, tangu mwezi Disemba mwaka jana mpaka sasa Juni," alisema.

Wakati wanawasilisha malalamiko yao, baadhi ya wananchi wa kijiji hicho waliovunjiwa nyumba na wengine kuchukuliwa mashamba yao, walisema hali hiyo inawakosesha amani kwa kuwa mara kwa mara wanachukuliwa maeneo yao na hakuna kinachoendelea.

"Tunaomba mkuu wa wilaya aje atuambie. Tumekuwa tukinyanyasika kwa kuchukuliwa maeneo yetu. Kuna kijana kidogo angefia humo ndani jana, maana aliaga anakwenda kulala,

"Lakini ni Mungu tu amemuepusha, kama hivi nyumba imevunjwa na kubomolewa, tunaomba tujue kama hatutakiwi kuishika kwenye maeneo haya watuhamishe tumechoka kunyanyaswa," alisema Subira Bakari.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Michungwani, Hamisi Chalo, akiwa kiongozi wa eneo hilo, hakuwahi kupokea taarifa zozote kuhusu kubomolewa kwa nyumba hizo, huku akionba serikali ya wilaya kuingilia kati suala hilo.

"Eneo hili liko Michungwani lakini huyo Askofu aliuziwa na watu wa kijiji cha Ugweno. Sasa watu walipoona amevamia na kubomoa wakaja Michungwani lakini mimi sina taarifa na hilo zaidi nauachia uongozi wa wilaya" alisema Chalo.

MAKALA

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA

# Allan Quatermain, kitabu kilichowapa vijana 'uchizi', asiyekisoma siyo mjanja

## -Masela walipagawa nacho, mabaharia ndiyo kabisaa!

**Na Adam Fungamwango**

MKUU, mkuu wa zamani. Mkuu, mkuu! Baba! Makumazahn, mzee mwindaji, muuaji wa tembo, mla simba, mwerevu akeshaye! Hodari, mwepesi! Ambaye risasi zake kabisa hazikosi shabaha, apigaye shabaha ya kweli, rafiki mwaminifu.

Mkuu! Baba! Ile methali ya kikwetu isemayo. Milima haikutani lakini wanadamu hukutana,' ni ya kweli kabisa na yenye busara.

Tazama! Tarishi alikuja toka Natal, akalia, 'Makumazahn amekufa! Nchi haitamwona Makumazahn tena.' Haya yalitokea zamani sana.

Na sasa, tazama hapa katika nchi ngeni ya harufu mbaya namwona tena Makumazahn, rafiki yangu.

Ndiye bila shaka. Manyoya ya mzee mbweha yameingia mvi; lakini macho yake na meno yake ni makali kama zamani.

Mkuu unakumbuka jinsi ulivyoipenyeza risasi kwenye jicho la nyati aliyekuwa akishambulia?

Unakumbuka unakumbuka?" Ni maneno yasiyosahaulika kwa vijana wa zamani ambao kwa sasa wameshakuwa watu wazima.

Maneno haya yanatoka kwenye kitabu maarufu sana enzi hizo cha simulizi za Allan Quaterman.

Kwa bahati mbaya siku hizi vijana wengi si wasomi wazuri sana vitabu kama ilivyo zamani.

Uchunguzi wangu mdogo ni kwamba, vijana wengi wa kisasa ni wavivu kusoma, badala yake wanapenda sana kuangalia. Wanapenda zaidi kuangalia filamu kuliko kusoma. Kuna utofauti kidogo kati ya kuangalia na kusoma. Filamu huonyesha moja kwa moja mazingira yaliyopo na kwa sababu mtu anaangalia hafikirishi zaidi ubongo.

Na wanaoangalia wote wanakuwa wanaona kitu kile kile. Lakini wanaosoma riwaya au hadithi, kila mtu anatengeneza taswira kivyake kichwani.

Kijana yoyote zamani ili akamilike kuwa mjanja ni lazima asome vitabu. Kuna vya watoto, halafu vya vijana. Kijana anapofika umri kuanzia miaka 15, anaanza kuvisoma. Vipo vingi, lakini leo tutaanza na kitabu kimoja maarufu mno cha 'Allan Quaterman'.

Sidhani kama vijana wa enzi hizo ambao kwa sasa ni watu wazima hawajavisoma. Nafikiri asilimia 90 ya vijana wengi wa Kitanzania miaka hiyo wamekisoma. Na hata asilimia ndogo iliyobaki ambao hawajakisoma, lakini watakuwa wamekipitia angalau kurasa tatu nne, au nusu. Hata kama vyote hivyo mtu hajapitia, lakini atakuwa anasikia habari au masimulizi ya kitabu hicho.

Nadhani ndiyo kitabu maarufu zaidi enzi hizo. Kilitungwa na mzungu mmoja anaitwa Sir.H Rider Haggard kwa lugha ya Kiingereza mwaka 1887, lakini kilitafsiriwa Kiswahili na kutoka Januari Mosi mwaka 1955 na kuondokea kupendwa sana hapa nchini, wakati huo ikiitwa Tanganyika na hata baada ya Uhuru, ikaitwa Tanzania.




Kitabu cha Allan Quatermain kilitengenezewa filamu ambayo ilizinduliwa mwaka 1986 nchini Ujerumani na hii ndiyo taswira ya mastaa ndani ya picha hilo.

Ni simulizi au kisa cha mwindaji wa tembo Bwana Allan Quatermain au kwa jina lingine Makumazan.

Huyo jamaa alikuwa na wasaidizi wake Msolopagazi, ambaye alikuwa na shoka lake kali alilolibatiza jina la Inkoskazi. Pia kulikuwa na wahusika wengine kama Bwana Henry Curtis na rafiki yake Sir Good. Kwenye riwaya hiyo, anapatikana bibi mmoja mchawi anaitwa Gagula.

Vijana wa kisasa, wakimhisi mtu machawi, wanamwita 'kikagula', lakini sidhani wengi wanajua jina hilo limetokea wapi. Ni kwenye kitabu hicho ndipo alipopatikana kibibi hicho Gagula ambaye ndiye jina lake, lakini akiwa na sifa ya uchawi, ndiyo ukazuka msamiati kwa vijana wa sasa.

Ni miongoni mwa riwaya zinazoonyesha au kusimulia ujasiri na ushujaa wa hali ya juu sana.

Riwaya hii ni moja kati ya riwaya chache duniani yenye maneno yenye hisia kali ambayo yanaingia ndani ya moyo na ubongo wa mtu na kumfanya abadilike.

Hapo ndipo baadhi ya watoto walianza kubalika na kuwa watukutu, wengine wagomvi, wababe, watemi, ujasiri na mashujaa pia.

Kitabu hiki kiliwabadilisha baadhi ya vijana kutumia vibaya maneno yaliyomo kwenye riwaya hiyo na kikapigwa marufuku kwenye miaka ya 1970. Kutokana na hali hiyo kikaacha kuchapishwa na watu wakawa wanaazimana tu vilivyopo. Hata hivyo kwa sasa vipo na vinauzwa kwenye maduka mbalimbali ya vitabu, ingawa si vijana wengi wanaojua hilo.

Kwa wale vijana wa zamani, walikuwa wazikariri baadhi ya maneno yaliyomo kwenye riwaya hiyo.

Hautoonekana mjanja kama kijana hautokariri baadhi ya mistrari iliyomo kwenye riwaya hiyo ya kale.

Vijana walikutana wakakati mwingine na kushindana, kila mmoja akitoa mistari yake aliyoikariri kwenye kitabu hiyo, hivyo kuwa burudani tosha kwa wale wanaowasikiliza.

Hadi leo hii ndiyo riwaya ambayo vijana wa wakati huo ambao kwa sasa wengi wao ni watu wazima, wazee na vikongwe na huenda wakawa wana matatizo ya kusahau, lakini hawawezi kusahau baadhi ya mistari au maneno yaliyomo kwenye kitabu hicho.

"Tu tayari! Tunainoa midomo yetu kama tai, mikuki yetu inang'aa katika miali ya Jua; twaitikisa mikuki yetu tuna njaa ya kupigana. Nani anayekuja kumwamkia Inkosikazi? Nani anataka kumbusu yeye ambaye matunda ya kubusu kwake ni kufa? Mimi Gotagota, mimi mwuaji, mimi mwenye mbio, mimi Umslopagaas mwenye shoka, wa kabila la Kizulu, mkuu wa kikosi cha Nkomabakosi: mimi Umslopogaas, mwana wa ulimi wa Mfalme, mwana wa Makedama, mtoto wa Mosilikaatze, mimi, wa damu ya Mfalme Chaka, mimi, mshindi wa wasio shindika, mimi nawaita kama kulungu aitwavyo, nawakaribisha, nawangojea.

Aha! Ni wewe, ni wewe! Kama wengi wengine walivyofanya, nawe utajiinamisha mbele ya Inkosikazi kama walivyofanya wengi wengine. Ndiyo, cheka, cheka! Usiku wa kesho, fisi watakuwa wanacheka na huku wanavunja na kuzitafuna mbavu zako."Hii ni moja ya nukuu kweye kitabu hicho.

"Nakufa, nakufa lakini vilikuwa vita vya Kifalme. Wako wapi wale walioipanda ngazi kuu? Siwaoni. Wewe upo Makumazan, au umekwisha nitangulia katika mahali pa giza ninakokwenda mimi? Damu inanipofusha - mahali panazungukazunguka, nasikia ngurumo ya maji, ninaitwa!" "Pigo moja, pigo moja takatifu."

Hii ni baadhi ya misemo maarufu ya kishujaa na kijasiri inayonukuliwa sana na wasomaji ndani ya riwaya hiyo. Wewe una msitari wako umeukariri?

**Tume meseji 0716 350534**

HABARI KIMATAIFA

# Marekani yaitaka Israel kuwataja waliouawa

**WASHINGTON,** MAREKANI

BAADA ya shambulizi lililowaua Wapalestina 35 waliojihifadhi katika jengo la shule, Marekani imeitaka Israel kuweka wazi kuhusu tukio hilo.

Ndege moja ya jeshi la Israel ilitupa makombora katika shule ya kati iliyoko Ukanda wa Gaza ambayo kipindi hicho ilijaa watu waliokimbia mapigano.

Waandishi wa habari wa eneo hilo waliambia BBC kuwa ndege ya kivita ilikuwa imerusha makombora mawili kwenye madarasa yaliyoua juu ya jengo la ghorofa ya shule ya wakimbizi ya Nuseirat mjini Gaza.

Awali, jeshi la Israel lilisema lilifanya shambulizi hilo kwa usahihi kwenye kiwanja cha Hamas katika shule hiyo, lakini ofisi ya vyombo vya habari vya serikali ya Gaza inayoongozwa na Hamas ilikanusha madai hayo.

Katika taarifa ya serikali ya Marekani, iliita Israel iwatambue na kutoa orodha hadharani majina ya wapiganaji wa Hamas iliosema wamewaua.

Jeshi la Israel huwa linawatambua wanamgambo inaowalenga katika mashambulizi ya anga lakini ni nadra kwa Marekani kuihimiza kufanya hivyo.

Katika taarifa yake, jeshi la Israel lilidai wanamgambo 20 hadi 30 waliokuwa wakiwalenga waliuawa na litatoa majina ya wale wanaoamini kuwa wamewaua.

Msemaji wa idara ya serikali ya Marekani, Matthew Miller alisema wameahidiwa hayo yote yatafanyika ili kupata hakikisho

Msemaji wa jeshi la Israel, Daniel Hagari, alitoa majina ya wapiganaji tisa wa Hamas na Islamic Jihad aliosema wameuawa katika shambulizi hilo.

Alisema zaidi watatambuliwa baada ya kuthibitisha taarifa zao.

Miller alisema Marekani imeona ripoti kwamba watoto 14 waliuawa katika shambulizi hilo.

"Ikiwa ni kweli kwamba watoto 14 waliuawa, hao sio magaidi, na kwa hivyo serikali ya Israel imesema itatoa taarifa zaidi juu ya shambulizi hilo.Tunatarajia watakuwa wawazi kabisa katika kuweka taarifa hizo hadharani." alisema. Vifo hivyo vimetokea wiki moja baada ya watu 45 kuawa katika shambulio la Israel katika mji wa Rafah.

Wakati huo huo, Kiongozi wa Hamas, Osama Hamdan alisema hawajapokea mapendekezo ya makubaliano ya kusitisha mapigano yaliyopendekezwa na Rais wa Marekani Joe Biden.

Wiki iliyopita, Biden aliwasilisha kile alichosema kuwa ni pendekezo la Israel kutekelezwa katika hatua tatu zitakazopelekea kumalizika kwa vita, kuachiliwa kwa mateka, na kujengwa upya kwa Ukanda wa Gaza bila kuwepo kwa Hamas madarakani.

Lakini Osama Hamdan aliambia shirika la Agence France-Presse kwamba hakuna pendekezo, bali ni maneno ambayo Biden alisema katika hotuba yake.

Alisema Biden alijaribu kuficha hatua ya Israel kukataa makubaliano yaliyowasilishwa hapo awali mnamo mwezi Mei na kuidhinishwa na Hamas.

Hamdan pia aliweka wazi kuwa Hamas iko tayari kukubali makubaliano yoyote yatakayofanikisha matakwa ya kimsingi ya kundi hilo ya kusitisha mapigano Ukanda wa Gaza na kuondoka kwa vikosi vya Israel katika maeneio yote ya Ukanda huo.

**BBC**



Wapiganaji wa kikosi cha wanamgambo cha RSF nchini Sudani wakiwa na vifaa vyao vya kijeshi katika jiji la Khartoum.
**PICHA: AP**

# Rais Ramaphosa akubali serikali ya muungano

**PRETORIA,** AFRIKA KUSINI

RAIS wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa, ametangaza rasmi kwamba chama chake cha African National Congress (ANC) kitaunda serikali ya umoja wa kitaifa na vyama vingine.

Katika uchaguzi mkuu wa wiki iliyopita ANC ilipata ushindi wa asilimia 40 ya kura kwa kujinyakulia viti 158 katika Bunge la Afrika Kusini, idadi ambayo haiwezi kuunda serikali.

Baada ya majadiliano ya saa10 na viongozi wakuu wa ANC, Rais Ramaphosa alitoa kauli ya kukiri kwamba chama chake kinahitaji washirika ili kuunda serikali ya mseto.

Kiongozi huyo alisema mazungumzo hayo yataimarisha kazi ya kujenga upya uwiano wa kijamii katika jamii iliyoshuhudia uchaguzi wenye migawanyiko.

Alihimiza pande zote lazima zijitolee katika ujenzi wa taifa kwa pamoja, na kusisitiza umuhimu wa kuheshimu katiba ya nchi na utawala wa sheria, haki ya kijamii, usawa, utu wa binadamu na kutokuwa na ubaguzi wa rangi na jinsia.

"ANC inabainisha kuwa tuna tofauti za kiitikadi na kisiasa na vyama kadhaa katika mazingira yetu ya kisiasa. Hata hivyo, hatutazuia uwezekano wa kufanya kazi na chama chochote ili mradi ni kwa maslahi ya umma na inazingatia kanuni nilizozieleza," alisema.

Tayari ANC imefanya mazungumzo na vyama vitano vya siasa, ambavyo ni EFF, Inkatha Freedom Party (IFP), Democratic Alliance (DA), National Freedom Party (NFP) na Patriotic Alliance (PA).

Awali, chama cha Inkatha Freedom Party (IFP) kilitangaza kwamba hakipingi wazo la kuunda serikali ya umoja wa kitaifa.

Chama cha Umkotho Wesizwe, ambacho kimepata asilimia 14.6 ya kura zote, kimekataa matokeo ya uchaguzi na kutishia kususia bunge.

**DW**

# Russia yapeleka meli za kijeshi Cuba

**HAVANA,** CUBA

MELI nne na manowari ya kivita kutoka Russia zinatarajiwa kuwasili nchini Cuba, siku chache baada ya Marekani kutangaza kuruhusu silaha zake zilizopelekwa Ukraine kushambulia ndani ya nchi hiyo.

Serikali ya Cuba ilitangaza juzi kuwa meli hizo za kivita za Russia, pamoja na manowari za kijeshi zitawasili katika mji mkuu wa Havana wiki ijayo.

Maofisa wa Cuba walisema hatua hiyo inatokana na kuwepo kwa uhusiano ya kirafiki na wa kihistoria kati ya mataifa hayo mawili.

Wakati meli hizo zikiwa safarini kuelekea Cuba, mvutano umeongezeka kuhusu msaada wa kijeshi wa nchi za Magharibi kwa Ukraine.

Wizara ya mambo ya nje, ilisema meli hizo zitakuwa nchini humo kwa siku sita kuanzia Juni 12 na hakuna meli yoyote iliyobeba silaha za nyuklia.

Tangazo hilo limetolewa siku moja baada ya maofisa wa Marekani kueleza kuwa wamekuwa wakifuatilia meli za kivita za Russia na ndege zilizotarajiwa kwenda Caribbean kwa ajili ya luteka za kijeshi.

**DW**

HABARI KITAIFA

# Waziri atoa siku 90 wathamini mihuri kidijiti

**Na Eleuteri Mangi,** DODOMA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa, ametoa siku 90 kwa Bodi ya Usajili ya Wathamini (VRB) kuzindua mihuri ya wathamini ya kisasa yenye alama za kidijiti ili wananchi wajiridhishe kazi zao zinazofanywa na wataalamu waliosajiliwa kisheria.

Silaa alisema hayo jana jijini hapa wakati wa mahafali ya wathamini ya tatu ya Bodi ya Usajili wa Wathamini inayosimamiwa na Bodi ya Usajili wa Wathamini.

"Namwelekeza Mwenyekiti wa Bodi ndani ya siku 90 kuanzia leo (jana), napenda kuona bodi inazindua mihuri ya wataalam yenye barcode (msimbomilia) kwa maana ya kuwa na alama za ulinzi za kielektroniki ambao utaunganishwa na mfumo wenu wa kutambua wathamini ili kusimamia misingi ya taaluma na weledi katika kutekeleza majukumu yao," alisema.

Alisema mihuri ya wathamini itasaidia wananchi wa kawaida kuwatambua wathamini kwa kuwa kila mmoja atakuwa na alama ambazo hazitafanana na mwingine.

Waziri Silaa alisema hatua itakayowasaidia kutambua kuwa kazi hiyo imefanywa na mtaalam ambaye anatambulika kisheria na kumchukulia hatua za kinidhamu kama atakiuka taaluma yake na misingi ya kazi yake.

Aidha, Waziri Silaa aliwaasa wahitimu wa hao kufanya kazi yao ya Uthamini kwa kumtanguliza na kumheshimu Mungu na kuwatumikia watanzania katika kupata huduma za uthamini kwa haki kwa kufuata misingi ya taaluma na sheria za nchi.

Awali, akimkaribisha Waziri Silaa wakati wa uzinduzi wa bodi hiyo, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Mhandisi Anthony Sanga, aliwasisitiza wajumbe hao kusimamia taaluma na weledi katika kazi ya uthamini kwa mujibu wa taaluma yao.

Sanga alisema milango ya wizara iko wazi wakati wote, hivyo waendelee kushirikiana ili kuleta maandeleo endelevu kwa taifa na watu wake na kuleta mabadiliko chanya ambayo yataacha alama katika kipindi cha uongozi wao.

Mwenyekiti wa Bodi ya Usajili ya Wathamini, Zidikheri Mgaya, alimhakikishia Waziri Silaa na menejimenti ya wizara ushirikiano wakati wote wa kutekeleza majuku yao hatua itayowasaidia Bodi hiyo kusimamia maadili ya taaluma ya uthamini.

Mahafali hayo yalihudhuriwa na wahitimu 91 ambao wanatambuliwa na Bodi ya Usajili wa Wathamini ambao walikula kiapo cha uadilifu katika kutekeleza majukumu yao kwa haki.



Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, akionyesha silaha bandia zilizokuwa zikitumiwa kutekeleza uhalifu na viroba vya bangi vilivyokamatwa . **PICHA: IMANI NATHANIEL**

## Bil.10/- kujenga kituo jumuishi cha huduma mahakama

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

SERIKALI imetenga Sh. bilioni 10 kujenga jengo la ghorofa tatu la Kituo Jumuishi cha huduma za mahakama eneo la Msamala, Manispaa ya Songea.

Mwakilishi wa mkandarasi anayetekeleza mradi huo, Mhandisi Godfrey Mgwasa, alisema jana kuwa mradi huo ukikamilika utakuwa na majengo manne ambayo yatakuwa na mahakama zote na kwamba jengo hilo litakuwa la kisasa lenye lifti mbili.

Pia alisema jengo hilo litakuwa litatoa huduma kwa watu wote ambao si watumishi wa mahakama na kwamba litakuwa na mashine za kutolea fedha (ATM) ili kurahisisha huduma kwa wananchi.

Mhandisi Mgwasa alibainisha kuwa alikabidhiwa mradi huo Desemba, mwaka jana na kwamba unatarajia kukamilika Septemba, mwaka huu, na hadi sasa utekelezaji umefikia asilimia 15 hyuku akikiri kwamba bado uko nyuma sana.

Akizungumza baada ya kukagua mradi huo, Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Ahmed Abbas Ahmed, alisema hajafurahishwa na kasi ndogo ya utekelezaji wa mradi huo, hivyo kumwagiza mkandarasi kuongeza nguvu kazi na vifaa ili mradi huo ukamilike kwa wakati.

"Ili kuhakikisha mradi huo unatekelezwa, mnatakiwa kufanya kazi usiku na mchana kwa kuwa hapa mna kila kitu ukiwemo upatikanaji wa umeme. Pia inatakiwa mnunue vifaa vya kutosha zikiwamo kokoto na vifaa vingine ambavyo vinaweza kutumika kwenye ujenzi," alisisitiza.

Mwaka 2023, serikali ilitia saini mikataba na kampuni nne yenye thamani ya Sh. bilioni 49 kwa lengo la kujenga vituo sita jumuishi vya kutoa huduma za mahakama katika mikoa ya Njombe, Katavi, Geita, Simiyu, Ruvuma na Songwe.

# Waliohamishwa hifadhini walia kukosa mawasiliano

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

WAKAZI wa Kata ya Miyombweni, Mbarali mkoani Mbeya, waliohamishwa kutoka ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, wamelalamikia eneo lao kutokuwa na huduma ya mawasiliano ya simu.

Hali hiyo ni kutokana na kutokuwapo kwa mnara wowote wa mawasiliano, jambo ambalo wamedai linakwamisha maendeleo.

Waliwasilisha malalamiko hayo juzi kwenye mkutano wa hadhara wa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, wa kusikiliza kero za wananchi na kuzitatua huku wakibainisha kuwa hawapati mawasiliano ya mtandao wowote wa simu hali inayowalazimu kwenda milimani na kwenye vichuguu.

Diwani wa Miyombweni, Jeremia Kisangai, alisema kuna eneo moja pekee ambalo wananchi wanaomiliki simu, wanakweda kusimama ili kupaa mtandao na kwamba liko mbali na makazi ya wananchi na ni porini hali ambayo alisema ni hatari kwa maisha yao.

Vilevile, alisema katika eneo hilo, ni vigumu kwa wananchi kuzungumza faragha na ndugu na marafiki zao kutokana na wengi wao kwenda kuwasiliana katika milima na vichuguu, hivyo hakuna siri ya mazungumzo.

"Hapo ulipo mkuu wa mkoa ukiangalia simu yako utakuta imeandika 'No service' (hakuna mtandao). Hali hiyo ndivyo ilivyo kwa wananchi wote wa eneo hili. Kule tunakokwenda kuwasiliana huwa hakuna siri maana kila ukienda unakuta watu wapo. Ukitaka uende peke yako labda iwe saa 8:00 usiku," alisema.

Kisangai aliiomba serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kuwasaidia wananchi hao kuondokana na kero hiyo kwa kuwajengea mnara jirani na eneo hilo huku akisema kuna baadhi ya wawekezaji wamejitokeza wanataka kuwekeza wakiwamo wanaotaka kujenga chuo cha utalii, hivyo mawasiliano ni muhimu.

Naye Asia Mkwama alisema wakati wanahamishwa na serikali kutoka katika kijiji cha Msangaji ya Zamani ambacho kilikuwa ndani ya hifadhi, walitawanywa katika maeneo mbalimbali, hivyo wanahitaji kuwasiliana na kujulishana taarifa mbalimbali zikiwamo za matatizo lakini wanashindwa kutokana na kukosekana kwa mtandao.

Alisema wengi wanshindwa kumiliki simu kwa sababu hazina maana kwao na kwamba endapo watajengewa mnara, watafanya maendeleo ikiwamo kununua simu ambazo zitawasaidia kufanya mawasiliano na wanunuzi wa mifugo na mazao wanayozalisha.

# HADITHI

TAARIFA ya Jeshi la Polisi inatangaza kuokotwa na maiti ya msichana mzuri na mrembo mno Mariamu, maeneo ya Tabata pembezoni mwa barabara mapema alfajiri.

Alikuwa amevalia mavazi ya michezo. Alionekana alikuwa anakimbia, ametoka au anakwenda jogging.

Taarifa ya madaktari inasema alikufa kwa mshtuko wa moyo, hiyo inaonyesha kuwa alianguka wakati anafanya zoezi alfajiri ile. Ndugu wa marehemu walikataa ripoti, kwani inaonekana kama alipigwa na kitu kizito kilichonasibishwa na chuma kichwani, kilichosabisha kuwa na tundu kichwani.

Ndugu wanaliomba Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi wa kina ili kugundua ukweli na wanaapa kuwa kama halikufanyika hilo, damu ya ndugu yao haitoenda bure. Kwani kuna nini? Kila nakala yako ya gazeti la Nipashe, itakupeleka kwenye ukweli wa jambo hili.

# Damu ya Mariamu-16

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

Mariamu alimtazama Kamal kwa dakika moja nzima bila kuongea kitu chochote, halafu akamuuliza.

"Hivi wewe mzima kweli?" "Mzima kama chuma cha pua." "Sasa haya maneno unayoongea yanatoka moyoni mwako, au umeambiwa uyaseme?" "Yanatoka moyoni mwangu kwa sababu hata nami naupenda uhai wangu." "Wamekufuata na kukutishia?"

"Mariamu, nimepokea meseji za vitisho kutoka kwa watu tofauti tofauti ambao sijajui na kila mara wanafanya hivyo. Na ukienda kuangalia zile namba kwenye simu hazionyeshi jina la mtu yoyote, na hata ukipiga hazipatikani. Kwa hiyo hapa unaponiona maisha yangu yapo hatarini. Siku yoyote na muda wowote naweza kuuawa."

Mariamu akaangua kicheko ambacho hakikuwa halisi. "Yaani unaupenda uhai wako kuliko mimi ninavyoupenda wangu?" "Kwa nini unaongea hivyo halafu unacheka?" Kamal naye akauliza.

"Kama kuogopa kifo basi mimi ningekuwa namba moja. Mimi nina meseji nyingi za vitisho zaidi yako. Nimetishiwa mimi kuuawa ili nikuache, nimewaambia nyie niueni tu, lakini hilo haliwezekani. Wamesema watakuua ili wanichukue kama hizo ulizonazo, nimewaambia hata mkimuua, mtakayempata ni marehemu Mariamu, siyo aliye hai, kwa sababu kama akifa Kamal na mimi najiua."

Na kwa uthibitisho alimuonyesha baadhi ya meseji ingawa si zote. "Ina maana hata mimi hapa nipo hatarini kuuawa. Kwa sababu kama nimewaambia hivyo na wananitaka nimewakataa, na watu wenyewe wengi ni wafanyabiashara, matajiri, wanasiasa na watu wenye ushawishi kwenye jamii ambao hata wakikumaliza wanaweza wasipatikane na wakipatana wasifungwe, wanaweza kuniua hata mimi ili tukose wote." Maneno hayo walimfanya Kamal kushusha pumzi. Presha ikamshuka. Akajiona kama ni mtu asiyefaa kuwa na mwanamke kama yule Yaani kutishwa ndiyo atake penzi livunjike, wakati mwenzake, mtoto wa kike amekomaa na kukubali kama wanataka kumuua wafanye hivyo na wakimuua mchumba wake wasidhani kama watafanikiwa, badala yake atajimaliza. Kwanza ilimtoa simanzi, aibu, lakini pia aligundua mpenzi wake pamoja na urembo wote na kutakiwa na watu wenye mamlaka, pesa na ushawishi lakini bado ameendelea kumpenda yeye na kumthamini. Akapeleka mikono na kumkumbatia mpenzi wake, huku machozi yakimtoka "Nisamehe mpenzi wangu, sikujua hilo, kumbe unanipenda sana!"




**Kingine kilichomuacha hoi ni baada ya ndugu kuchachamaa, taarifa ya pili ya uchunguzi ikaja kumuonyesha yeye kuwa ndiye muuaji. Na amefanya hivyo kutokana na wivu wa mapenzi kwani mchumba wake alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na wanaume wengine. Baada ya kuona meseji ndiyo ugomvi ukaanza, akamuua na usiku kwenda kumtupa kwenye mtaro pale Tabata baada ya kumvalisha nguo za michezo.**

Mariamu hakuonekana kukasirika kama alivyodhani Kamal. Alileta ushirikiano. Akamkumbatia pia.

"Jiamini baba, wewe ndiye unatakiwa kuwa mlinzi wangu, wewe ni mwanaume, haya maneno nilitakiwa niseme mimi..." "Basi, basi mama, nimefuta wazo langu, kiukweli tu lilikuwa la kijinga, kama ni hivi nitaendelea kuwa na wewe milele, niko tayari kufa kwa ajili yako, kama ambavyo wewe umewaambia jamaa na meseji umeiona uko tayari kufa kwa ajili yangu." Mapenzi yaliendelea kama kawaida. Lakini kila mmoja alikuwa anajua moyoni mwake kuwa wana maadui. Na ni watu wenye uwezo, na ushawishi kwenye jamii.

Hata kupotea kwa Mariamu na kesho yake maiti yake kuonekana, Kamal alianza kuhisi ni mambo yale yale waliokuwa wakiyasoma kwenye meseji.

Kubadilishwa mara mbili kwa taarifa za uchunguzi wa kifo hicho, kulimthibitishia kuwa ni kweli wale jamaa waliokuwa wanamtumia yeye meseji na mpenzi wake pia si watu wa mchezo mchezo.

Awali ilionekana alianguka kutokana na mshtuko wakati akikimbia jogging maeneo ya Tabata. Kuvishwa nguo za mazoezi wakati hakuwa na nguo hizo kulizidi kumuonyesha kuwa ni watu waliojipanga kupoteza ushahidi.

Kingine kilichomuacha hoi ni baada ya ndugu kuchachamaa, taarifa ya pili ya uchunguzi ikaja kumuonyesha yeye kuwa ndiye muuaji. Na amefanya hivyo kutokana na wivu wa mapenzi kwani mchumba wake alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na wanaume wengine. Baada ya kuona meseji ndiyo ugomvi ukaanza, akamuua na usiku kwenda kumtupa kwenye mtaro pale Tabata baada ya kumvalisha nguo za michezo.

Leo hii amechiwa yeye zigo lote la mauaji ambayo hakuyafanya. Anahangaika kujificha, jamii yote ikiomuona ni muuaji, mwenye hatia ya kunyongwa mpaka kufa. Amelazimika kufanya hivyo kwa sababu haitotokea siku ambayo jamii itajua ukweli kama yeye mwenyewe hatokuwa hai, au uraiani.

Mawazo yalirejea na kujikuta bado yumo kwenye chumba alichopanga kwenye hoteli moja Ubungo.

Akaamua kujipumzisha. Alijua kabisa kuwa kwa sasa maisha yake hapo hatarini. Kuna upande mmoja unamsaka ili umtie mbaroni kwa shtaka la mauaji, mwingine unamtafuta ili kufuta ushahidi.

Japo upande huu haupo dhahiri, lakini alijua waliomuua Mariamu watakuwa wanamsaka ili wammalize kwa sababu wanajua ni yeye tu ndiye anayefahamu kuwa hajamuua.

Kitendo cha kuwa hajamatatwa mpaka sasa hakiwezi kuwapa usingizi waliofaya udhalimu huo, hivyo ili wakae kwa amani ni lazima wahakikishe, ama anatiwa mikononi wa polisi, au wanamuwahi kwa kummaliza. Kitu pekee ambacho anajivunia ni kwamba pande zote mbili hazijui pamoja na kwamba ametoroka, hawajui nini anataka kufanya. "Akili yao wao wanajua mimi nakimbia huku na kule kujifichaficha tu bila mpango, wamenia." Akajisemea moyoni.

Asubuhi kulivyokucha aliondoka hapo moja kwa moja hadi kwenye zahanati moja maeneo ya Ilala.

Alimkuta mhudumu, akamwambia anajisikia vibaya, hivyo anaomba kitanda alazwe.

"Kwani unajisikiaje, huna nguvu?" "Siyo kama sina nguvu na kizunguzungu juu." Kamal alimjibu nesi aliyempokea. Hakukuwa na daktari kwa muda huo. Alipokuja alimpima lakini hakumkuta na ugonjwa wowote.

"Nadhani ni uchovu na kufanya kazi bila kumpumzika, lakini tumekupima kila kitu, unaonekana hauna tatizo." "Sawa lakini mimi dokta bado najisikia vibaya, tena kichwa ndiyo kabisa." "Basi endelea kumpumzika." Alipoondoka alipoondoka, alimwita nesi na kumwambia lengo lake ni kupumzika pale kwa siku tatu. Kabla nesi hajauliza sababu, alitoa noti tatu za shilingi efu kumi, akamkabidhi. Nesi akatabasamu. "Nataka nipumzike kwa sababu nina msongo wa mawazo, sitaki kurudi uraiani, nina matatizo kwenye familia yangu. Pia naomba unifunge bandeji kichwani kama mtu aliyeumia ili sura yangu usionekana vyema. Ndugu zangu wanaweza kunitafuta mahospitalini na zahanati wakanikuta hapa." Nesi akatii. Lengo halikuwa hilo. Ilikuwa ni kuishi pale kwa siku tatu bila bughuza. Polisi wanaweza kumsaka mhalifu sehemu zote, lakini siyo hospitalini na zahanati. Hata wanaomsaka hawawezi kuwa na wazo kuwa atakuwa anaishi hospitalini. Akili yake ilimtuma baada ya siku tatu atarejea kwenye hoteli aliyopanga Ubungo kuchukua mizigo yake ili ahamie sehemu nyingine.

*Itaendelea Jumamosi*

# KARATA YA MWISHO JKT KUBAKI LIGI KUU

**Na Shufaa Lyimo**

KLABU ya JKT Tanzania leo ina karata muhimu ya kuamua hatma yao ya kubaki Ligi Kuu msimu ujao itakapoumana na Tabora United kwenye mchezo wa marudiano wa 'Play Off' utakaochezwa kwenye uwanja wa Meja Jenarali Isamuhyo.

JKT inapewa nafasi kubwa ya kubaki Ligi Kuu baada ya matokeo mazuri ya bao 4-0 waliyoyapata kwenye mchezo wa kwanza ugenini.

Endapo JKT Tanzania itapata sare au ushindi wowote itakuwa imejihakikishia msimu ujao kuendelea kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Malale Hamsini alisema amewajenga kisaikolojia wachezaji wake ili waweze kupata ushindi katika mchezo huo.

Alisema amewataka kusahahu matokeo ya mchezo wa kwanza na waanze upta kusaka ushindi ili wajihakikishie kubaki Ligi Kuu.

"Wachezaji wangu wana morali ya juu kuelekea kwenye mchezo huo ambao utakuwa na upinzani mkubwa, nimewaambia wasahau ya nyuma waangalie mbele zaidi, huu mpira wa miguu lolote linawezekana," alisema Malale.

Alisema amefanyia kazi mapungufu aliyoyaona kwenye kikosi chake kwenye mchezo uliopita na anafuraha kuona kila mchezaji anautamani mchezo huo wa leo.

"Kikubwa nawaomba mashabiki wa JKT na wapenzi wa mpira kujitokeza kwa wingi kushuhudia mchezo huu na kutupa hamasa kutimiza malengo yetu," alisema Malale.

## Zimamoto yakoleza moto Ligi Kuu Z'bar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

ZIMAMOTO SC imeendelea kukoleza moto wao kwenye michezo ya Ligi Kuu ya Zanzibar baada ya juzi kuibuka na ushindi wa mabao 4-1 dhidi ya Maendeleo FC na kupanda mpaka nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi hiyo.

Mchezo huo uliokuwa na msisimko ulichezwa kwenye uwanja wa Finya kisiwani Pemba.

Matokeo hayo yameifanya Zimamoto kufikisha pointi 55 na kuishusha KMKM yenye pointi 54 kwenye nafasi ya pili katika msimamo huo unaoongozwa na JKU SC wenye pointi 62.

Baada ya mchezo huo, Kocha wa Zimamoto SC, Mohamed Hilali alisema sasa nguvu zao wanaelekeza kwenye michjezo minne iliyobakia kabla ya kumalizika kwa ligi hiyo.

Alisema anajua michezo hiyo haitakuwa rahisi kwa kuwa kila timu inataka kumaliza nafasi nzuri na za juu katika hivyo wamejipanga kukabiliana nayo.

Aidha, alisema anashukuru kwa sasa kikosi chake mpaka kipo vizuri na bado Kina matumaini ya kupambana katika kuhakikisha wanamaliza vizuri msimu huu.

> "Bado Tunaendelea na mapambano ya kuhakikisha hatupotezi lengo letu, wachezaji bado wanahamasa na kila mchezo tunaoshuka uwanjani wanaendelea kujituma, tutapambana mpaka mwisho wa msimu tuone tutakuwa wapi," alisema Hilali.

Alisema baada ya kutolewa kwenye kuondolewa kwenye Kombe la FA, kwa sasa matumaini yao yapo kwenye ubingwa wa Ligi Kuu peke yake.

Katika hatua nyingine, kwenye michezo ya ligi hiyo juzi, kwenye uwanja wa Mau A, New City FC ilikumbana na kipigo cha mabao 3-0 kutoka kwa Maafande wa KVZ FC.

## KIKAPU

**Kocha wa vijana wa Mpira wa Kikapu, Colimel Msuya, akitoa maelekezo kwa wachezaji wake wakati walipokuwa wakifanya mazoezi katika Uwanja wa michezo wa Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam jana. PICHA: JUMANNE JUMA**



# BMT YATAKA TAIFA KIKAPU KUPAMBANA

**Na Shufaa Lyimo**

BARAZA la Michezo la Taifa (BMT) imeitaka timu ya taifa ya mpira wa kikapu kwa vijana chini ya miaka 18, kwenda kupambana na kuipeperusha vyema bendera ya Tanzania kwenye mashindano ya Afrika yanayoanza leo nchini Uganda.

Mashindano hayo ya wiki moja yanayohusisha nchi mbalimbali za Afrika yatafikia tamati Juni 17, Jijini Kampala.

Akizungumza na wachezaji hao muda mfupi kabla ya kuelekea Uganda, Ofisa Michezo wa BMT, Charles Maguzu, amewataka kufuata maelekezo na mbinu walizopewa na benchi lao la ufundi kwani zitawasaidia kufanya vizuri katika mashindano hayo.

„Nendeni mkapambane mrudi na ushindi nyumbani, kwa maandalizi ya muda mrefu mliyoyafanya naamini mtakwenda kufanya vema," alisema Maguzu.

Aidha, Maguzu aliwapongeza wachezaji wote waliopata nafasi ya kuitwa kwenye timu hiyo kutokana na uwezo mzuri waliouonyesha katika mashindano mbali mbali ya ndani na nje ya nchi.

Kwa upande wake Ofisa Habari wa Shirikisho la mpira wa kikapu Tanzania (TBF), Mary Arthur alisema malengo yao ni kwenda kushindana na si kushiriki.

„Tumefanya maandalizi ya kutosha kuhakikisha timu yetu inakawenda kuipeperusha vizuri bendera ya Taifa kupitia mashindano hayo kutokana na morali inayoonyeshwa na kila mchezaji," alisema Mary.

Alisema timu hiyo ambayo iliondoka jana Ijumaa imeshirikisha timu ya wanaume pamoja na wanawake.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**OSIMHEN KUPISHANA NA LUKAKU**

UHAMISHO wowote wa Romelu Lukaku kwa Napoli utatokea tu ikiwa watafanikiwa kumuuza mshambuliaji wa Nigeria Victor Osimhen mwenyewa miaka 25. ***(Times)***

**DOMINIC KUONDOKA BURE**

KLABU ya Everton ina hatari ya kumpoteza mshambuliaji wa England, Dominic Calvert-Lewin kwa uhamisho wa bure mwaka 2025 baada ya kusitishwa kwa mazungumzo ya mkataba mpya kwa mchezaji huyo mwenye miaka 27. ***(Football Insider)***

**KLABU SITA EPL KUUZA**

KLABU sita za Ligi Kuu England, Chelsea, Aston Villa, Newcastle United, Everton, Nottingham Forest na Leicester zinakabiliwa kulazimika kuuza wachezaji kabla ya mwisho wa Juni ili kuzingatia Sheria za Faida na Uendelevu ***(Sky Sports)***

**SOLANKE NA KIPENGELE HURU**

MSHAMBULIAJI wa England na Bournemouth, Dominic Solanke mwenye miaka 27, ana kipengele cha kuachiliwa huru cha pauni milioni 65 katika mkataba wake. ***(Athletic)***

**MICHAEL OLISE KIPAUMBELE**

KLABU ya Chelsea imemfanya winga wa Crystal Palace na Ufaransa, Michael Olise mwenye umri wa miaka 22, kuwa mmoja wa walengwa wao wakuu wa uhamisho wa majira ya joto, huku The Blues wakiwa tayari kupambana na Manchester United ili kumnasa mchezaji huyo anayekadiriwa kuwa na thamani ya pauni milioni 60. ***(Standard)***

**UNITED, MADRID WAMGOMBEA YORO**

KLABU ya Manchester United wamewasilisha ombi la euro milioni 60 kumnunua mlinzi wa Lille, mwenye miaka 18, Leny Yoro, lakini wanakabiliwa na ushindani kutoka kwa Real Madrid wa kuwania saini ya kinda huyo wa Ufaransa.***(Marca)***

**MAATSEN ATAKIWA**

KLABU ya Borussia Dortmund inataka kumsajili beki wa kushoto wa Uholanzi, Ian Maatsen mwenye miaka 22, kwa mkataba wa kudumu baada ya kuonesha kiwango kizuri akiwa kwa mkopo lakini wanasita kufikia kiwango cha Chelsea cha pauni milioni 35. ***(ESPN)***

**HURZELER ATAJWA BRIGHTON**

KLABU ya Brighton imemuweka Fabian Hurzeler mwenye umri wa miaka 31 kwenye orodha yao kama kocha ajaye. Kocha huyo mzaliwa wa Marekani aliiongoza St Pauli kupanda daraja kutoka Bundesliga 2 msimu uliopita. ***(Telegraph)***

**POTTER KUREJEA**

BRIGHTON imefanya mazungumzo na bosi wao wa zamani, Graham Potter mwenye miaka 49, kuhusu uwezekano wa kurejea kufundisha timu hiyo. ***(Guardian)***

**GABRIEL AITAKA CORINTHIANS**

MLINZI wa kati wa Arsenal na Brazil, Gabriel mwenye miaka 26, amesema ni "ndoto yake" kujiunga na klabu ya Corinthians ya Brazil, timu ambayo amekuwa akiishabikia tangu akiwa mtoto.***(Mirror)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# LUKAKU AFUNGUKA KUHAMIA SAUDIA

●●●Ni mwaka mmoja tangu mshambuliaji huyo alipokataa kujiunga na klabu ya Al Hilal, lakini sasa...

**LONDON,** ENGLAND

ROMELU Lukaku amesema yuko tayari kucheza nchini Saudi Arabia ikiwa ni mwaka mmoja baada ya kukataa kuhamia Al Hilal.

Mustakabali wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 bado haujulikani kwa mara nyingine kwani vyanzo vimeiambia ESPN kwamba Chelsea wana nia ya kupata uhamisho wa kudumu kwa Lukaku baada ya kukubali kumtoa kwa mkopo mshambuliaji huyo kwa Inter Milan na kisha Roma katika misimu miwili iliyopita.

Lukaku anapokea kiasi cha pauni 325,000 kwa wiki huko Stamford Bridge na Chelsea wanataka kuondoa gharama hiyo kwenye bili yao ya mishahara huku wakichangisha fedha kwa ajili ya wachezaji wapya.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji amebakiza miaka miwili kwenye mkataba wake wa sasa na Chelsea na hivyo klabu hiyo inasita kuidhinisha uhamisho wa tatu wa mkopo huku ikitafuta kufidia pauni milioni 97.5 walizolipa kwa Inter Milan mwaka 2021.

Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba Chelsea ilijaribu kukubaliana na mpango wa Lukaku kujiunga na Al Hilal msimu uliopita wa majira ya joto, ikikubali ofa tu kwa Lukaku kisha kukataa pendekezo hilo.

Hata hivyo, Lukaku sasa anaamini Ligi Kuu ya Saudia inazidi kuimarika kufuatia kuwasili kwa nyota wengi wakubwa wakiwemo Cristiano Ronaldo, Neymar na Karim Benzema.

Alipoulizwa kwa nini mwanzo alisita, Lukaku aliiambia HLN: "Kwa sababu kila mtu alikwenda Saudi Arabia baada ya kusaini huko, niliogopa kwa muda.

"Sasa Saudi Arabia kiwango kitapanda watu wengi wanavyofikiria. Wanasoka wengi zaidi wataelekea kucheza huko.

"Pia kutokana na jinsi mashabiki wa huko wanavyopata uzoefu wa soka. Miundombinu bado inahitaji kuboreshwa, lakini klabu zote kubwa za Ulaya zinajua: ‚Saudi Arabia inakuja.' Tayari unaona hilo kwenye ndondi na gofu."

Akizungumzia uwezekano wa kuhama kipindi hiki cha kiangazi, Lukaku alisema, „Watu wengi wanapenda kuzungumza, labda kwa sababu sina wakala. Lakini nitaamua. Ninadhibiti hali yangu mwenyewe.

"Nitafanya chaguo sahihi na mara nitakapolielezea, kila mtu atakubaliana nami."

# GREALISH, MAGUIRE WATEMWA ENGLAND

**LONDON,** ENGLAND

GARETH Southgate amekihimiza kikosi chake kipya cha England kuungana baada ya nyota kadhaa wenye hadhi ya juu kuachwa nje ya kundi lao la mwisho la wachezaji 26 kwa ajili ya michuano ya Euro 2024.

Jack Grealish wa Manchester City, Harry Maguire wa Manchester United na James Maddison wa Tottenham Hotspur wote watakosa michuano ya msimu huu wa majira ya joto pamoja na wachezaji wawili wa Liverpool, Curtis Jones na Jarell Quansah, na Jarrad Branthwaite wa Everton na James Trafford wa Burnley baada ya Southgate kupunguza orodha yake ya muda ya wachezaji 33.


Hasa nusu ya kikosi cha wachezaji 26 ambacho Southgate alikipeleka kwenye Kombe la Dunia la 2022 nchini Qatar zaidi ya miezi 18 iliyopita wameachwa nyuma huku 12 kati ya waliochaguliwa hawajawahi kushiriki mashindano makubwa.

Kukosekana kwa Maguire kulichangiwa zaidi na jeraha la mguu ambalo Southgate alisema "bila shaka" lingemtoa nje ya hatua ya makundi.

Grealish na Maddison walipuuzwa kwa kupendelea kujumuisha washambuliaji wachanga, akiwemo Antony Gordon wa Newcastle United na Cole Palmer wa Chelsea, huku Kobbie Mainoo wa United na wawili wa Crystal Palace, Adam Wharton na Eberechi Eze wakichaguliwa licha ya kutokuwa na uzoefu.

Wachezaji wakonge, Jordan Henderson na Kalvin Phillips pia wameachwa nje ya kikosi hicho cha England.

"Kwa kweli, tuna mabadiliko mengi kutoka Qatar ikiwa utarudi nyuma hadi hapo," alisema Southgate.




"Uamuzi wa kuchagua kikosi daima ni wa wakati kwa wakati. Wakati mwingine unaweza kuunda tena kikundi zaidi kuliko vile ulivyokuwa ukitarajia miezi michache iliyopita lakini hiyo tayari imeleta njaa, ushindani na muhimu kwa sasa ni lazima tujifunge.

"Kuna baadhi ya wachezaji wamekaa nasi kwa muda mrefu, Kundi lazima lifanye kazi pamoja, lazima watambue kwamba tunapochagua timu 15 ambao wamekata tamaa watakuwa muhimu kwa kila mechi kwa sisi kufanya vizuri kwa sababu wengi wao watakuja kwenye mchezo.

"Kwa hiyo, baadhi ya vijana hawajapata uzoefu huo katika ngazi ya juu. Tumepata washindi wa chini wa Kombe la Dunia katika kundi hilo na washindi wa chini wa Euro kwa hiyo wana uzoefu wa mashindano na tuna wachezaji wazuri sana. Sina wasiwasi na wachezaji niliowachagua, tunapaswa kuyafanyia kazi katika wiki zijazo."

Grealish alianza mechi 10 pekee za Ligi Kuu msimu huu huku City wakishinda taji lao la nne mfululizo.

Maddison alitatizika kurejesha kiwango chake cha msimu wa mapema tangu arejee kutoka kwa jeraha mwishoni mwa Januari, akifunga bao moja pekee la Ligi Kuu dhidi ya Aston Villa Machi 10.

Kikosi kamili

Makipa: Dean Henderson, Jordan Pickford, Aaron Ramsdale

Walinzi: Lewis Dunk, Joe Gomez, Marc Guehi, Ezri Konsa, Luke Shaw, John Stones, Kieran Trippier, Kyle Walker

Viungo: Trent Alexander-Arnold, Conor Gallagher, Kobbie Mainoo, Declan Rice, Adam Wharton

Washambuliaji: Jude Bellingham, Jarrod Bowen, Eberechi Eze, Phil Foden, Anthony Gordon, Harry Kane, Cole Palmer, Bukayo Saka, Ivan Toney, Ollie Watkins

# Martinez: Copa America sio mwisho wa Messi

**FLORIDA,** MAREKANI

MLINZI wa Manchester United, Lisandro Martinez amesema timu ya taifa ya Argentina haichukulii michuano ya Copa America ya 2024 kuwa ya mwisho kwa Lionel Messi akiwa na La Albiceleste, akiongeza kuwa nahodha huyo anasalia kuwa mchezaji bora zaidi duniani.

Messi amesema itakuwa vigumu kwake kucheza Kombe la Dunia 2026, atakapofikisha umri wa miaka 39, ingawa kocha Lionel Scaloni amesema anaamini kuwa mshindi huyo mara nane wa Ballon d'Or anaweza kucheza michuano hiyo itakayoandaliwa Marekani, Canada na Mexico.

"Yeye ni mtulivu sana, zaidi ya kitu chochote anachofurahia siku hadi siku. Inapendeza kuwa hapa, sote tuna uhusiano mzuri," alisema Martínez akiwaambia waandishi wa habari wakati wa maandalizi ya timu huko Fort Lauderdale, Florida.

"Mtu anapokuwa hapa, ana furaha sana. Tunajisikia nyumbani, jambo ambalo ni muhimu. Hatuoni kama michuano yake wa mwisho na Argentina. Tunamwona akiwa na furaha, na kiwango cha kuvutia. Hilo ndilo ninaloweza kusema."

Scaloni aliunga mkono hilo akiwataka Waagentina kutozingatia ni lini Messi ataiaga timu ya taifa.

"Sisi Waagentina tuna furaha sana," aliiambia Telemundo. "Tayari tunafikiria siku ambayo Messi hayupo hapa wakati bado anacheza.

"Hebu tumfurahie na tutaona kitakachofuata. Nadhani anachofanya sasa hivi ni muhimu sana. Na kwa kila mtu, sio tu kwa Argentina, kwa sababu mwishowe Leo anacheza kwa wale wanaopenda mpira. Lakini siku moja kustaafu kwake kutatokea."

Messi amekuwa sehemu muhimu ya mafanikio ya timu ya taifa ya Argentina, akiwa nahodha na kushinda Copa América 2021 na Kombe la Dunia la FIFA la 2022.

Tangu alipocheza kwa mara ya kwanza mwaka 2005, fowadi huyo amefunga mabao 106 katika mechi 180 za kimataifa na kuwa mfungaji bora wa muda wote wa nchi hiyo.

Nyota huyo wa zamani wa Barcelona na Paris Saint-Germain bado yuko katika kiwango kizuri, akifunga mabao 11 na kuongeza asisti 12 katika mechi 12 za Inter Miami CF kwenye MLS msimu huu. Mkataba wake na Miami unaendelea hadi mwisho wa msimu wa 2025.

# Klabu za EPL zaunga mkono kuendelea kutumika kwa VAR

**LONDON,** ENGLAND

KLABU za Ligi Kuu England,EPL, zimepiga kura na kuunga mkono kwa wingi wa kura 19 kwa 1 kuendelea kutumika kwa mfumo wa usaidizi wa waamuzi kwa njia ya video (VAR) msimu ujao.

Wolves ilisababisha upigaji kura kuhusu matumizi ya VAR kwa msimu wa 2024-25 baada ya kuwasilisha rasmi azimio kwa Ligi Kuu mwezi uliopita.

Ili VAR iondolewe, klabu 14 kati ya 20 za Ligi Kuu zinahitajika kupiga kura ya kuunga mkono.

Lakini ni Wolves pekee iliyopiga kura ya kukataa.

Wolves imesema "imesikitishwa na matokeo ya kura" lakini imefurahishwa na "nia thabiti ya Ligi Kuu kuboresha VAR".

Ligi Kuu imejikuta katika shinikizo linaloongezeka la kutaka marekebisho ya VAR, iliyoanza kutumika mwanzoni mwa msimu wa 2019-20.

Wolves iliorodhesha sababu tisa za kujenga hoja ya pendekezo lake la kufutwa kwa VAR, ikiwemo madhara kuhusiana na ushangiliaji wa goli, uhasama dhidi ya waamuzi na urefu wa muda unahitajika kufikia maamuzi.

Wakati wa mkutano lilitolewa hakikisho kuwa kutaanzishwa mfumo wa kiteknolojia kuamua matukio ya kuotea wakati wa majira ya kipupwe, huku Ligi Kuu ikithibisha kuwa kutakuwepo matangazo kuhusu VAR wakati mchezo ukiendelea.

Matangazo wakati mchezo ukiendelea, yaliyotumika wakati wa fainali za Kombe la Dunia kwa wanawake 2023, yatahusisha waamuzi kuwaeleza mashabiki viwanjani baada ya maamuzi ya VAR.



HABARI MICHEZO

# AZAM YATHIBITISHA KUMNASA MSHAMBULIAJI MASHUJAA FC

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Azam FC, imethibitisha kumsajili mshambuliaji wa Mashujaa FC, Adam Adam, ikimpa mkataba wa mwaka mmoja kuitumikia timu hiyo akiwa mchezaji wa kwanza wa Kitanzania kusajiliwa na timu hiyo katika kipindi hiki.

Taarifa iliyotolewa na klabu hiyo imesema kuwa imemsajili mchezaji huyo kutokana na uwezo wake, kwani amepachika mabao saba msimu uliomalizika, pia alilelewa kwenye akademi yao.

Mwishoni mwa mwezi huu, klabu ya Mashujaa FC ilitangaza kuachana na mchezaji hiyo ikidai ni kwa makubaliano ya pande zote mbili, lakini taarifa ambazo gazeti hili liliripoti kutoka kwenye vyanzo ndani ya kikosi hicho chenye maskani yake Kigoma, mchezaji huyo alikuwa anaelekea Azam.

„Baada ya kucheza miaka 10 nje ya viunga vya azam Complex, hatimaye tumemrejesha kijana wetu.

Tunathibitisha kuwa tumeingia naye mkataba wa mwaka mmoja, tayari kabisa kuitumikia Azam FC msimu ujao, 2023/24,“ ilisema sehemu ya taarifa ya klabu hiyo kwa vyombo vya habari.

Mshambuliaji huyu ni moja ya zao la Akademi ya Azam FC, aliyojiunga nayo mwaka 2011 na kudumu mpaka mwaka 2014, akiwa chini ya Kocha, Vivek Nagul na kubeba baadhi ya mataji kadhaa ikiwemo la Rollingstone.

Adam, alianza kuwika alipokuwa na kikosi cha JKT Ruvu ambayo sasa ni JKT Tanzania mwaka 2020, kabla ya kutimkia Al Wahda Tripoli ya Libya mwaka 2021 ambako alikaa kwa muda mfupi na mwaka mmoja baadae akarejea nchini na kujiunga na Polisi Dodoma.

Hata hivyo hapo napo hakudumu sana na baadae kujiunga na Mtibwa Sugar kabla ya kujiunga na Ihefu Fc na baadae Mashujaa FC.

Adam anakuwa mchjezaji wa tano kusajiliwa na Azam katika kipindi hiki, lakini yeye anakuwa mzawa pekee kusajiliwa.

Mbali na nyota huyo, wachezaji ambao Azam tayari imewasajili ni beki wa kati, Yoro Mamadou Diaby na kiungo mshambuliaji Franck Tiesse, wote kutoka Stade Malien ya Mali.

Wengine ni Wacolombia, Jhonier Blanco kutoka Aguilas Doradas ya Rionegro, inayoshiriki Ligi Kuu nchini humo na kiungo mshambuliaji Ever Meza kutoka Leonnes.



Mchezaji wa timu ya Vijana ya JMK, Majdi Tamimu, akimiliki mpira huku akizongwa na mchezaji wa Tuangoma, Arafat Tichumu, kwenye mchezo wa kirafiki iliyofanyika kwenye Uwanja wa Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Uongozi Coastal wambana Matampi

**Na Faustine Feliciane**

UONGOZI wa klabu ya Coastal Union ya Tanga bado umeendelea kusisitiza golikipa Ley Matampi bado ni mali yao na kumtaka mkongo huyo kuonyesha mkataba wake wa mwaka mmoja anaosisitiza kuusaini kabla ya kuanza kuichezea timu hiyo msimu uliopita.

Mara baada ya kumalizika kwa Ligi Kuu Tanzania bara hivi karibuni, kumeibuka mvutano wa kimkataba kati ya uongozi wa klabu hiyo golikipa Ley Matampi wakivutana juu ya uhalali wa mkataba wa nyota huyo.

Golikipa huyo raia wa Kongo amekwa wazi kuwa amemaliza mkataba wa kuichezea timu hiyo kwa kuwa mkataba wake na timu hiyo ulikuwa wa mwaka mmoja.

Hata hivyo, uongozi wa Coastal Union ukiongozwa umemtaka golikipa huyo aonyeshe mkataba huo wa mwaka mmoja anaodai kusaini.

Akizungumza na Nipashe jana, Katibu Mkuu wa klabu hiyo Omar Ayoub,alisema hawana nia ya kumzuia Matampi kuondopka kama amepata timu, lakini wanataka tararibu na sheria zifuatwe.

„Sisi kama Coastal Union tunasema Matampi bado ana mkataba na sisi, sasa yeye kama anasema alikuwa na mkataba wa mwaka mmoja tu, auonyeshe, sisi nyaraka zote tunazo,“ alisema.

Alisema hata kama kuna timu inamuhitaji hawatasita kumruhusu kama watafuatwa na kukubaliana.

## Mo Dewji ‘afyeka’ wajumbe Simba

INATOKA UK. 24

kila mmoja amefanya hivyo kwa manufaa ya klabu.

„Ukweli ni kwamba hatukulazimishwa au kutakiwa kujiuzulu na mwekezaji, unawezaje kushinikizwa?, Ni mambo tu ya kwenye mitandao, kila mmoja ameteuliwa kwa wakati wake, ila kuna suala la kujitathmini, inawezekana tu kuwa jana (juzi) ilikuwa ni siku ya mwisho ya kujiuzulu, kwa taarifa tu ni kwamba mimi niliandika barua wiki moja iliyopita, wengine walishajiuzulu mwezi mmoja uliopita ni suala tu la uwajibikaji na kujitathmini si suala geni, ni namna tu ya kuipa taasisi nafasi ya kupumua,“ alisema.

Kutokana na hali hiyo, alisisitiza umoja na mshikamano uendelee huku akiwasihi wenzake wanaoondoka kuwapa ushirikiano watakaokuja ili kutengeneza Simba yenye mafanikio ndani na nje ya uwanja.

„Umoja na mshikamano ndiyo suala la msingi, niwasihi tu Wanasimba hiki ni kipindi cha mpito, ni vyema tukawa pamoja, tukashirikiana, tumeondoka ili kumpa mwekezaji wetu nafasi ya kuunda upya safu yake na kuipa ushirikiano kuanzia nje ya uwanja, tukifika ndani hata vijana wetu ambao tutakuwa tumewasajili watajua dhana ya nguvu moja ipo, watafanya vizuri,“ alisema.

Awali, taarifa zinasema Mo, aliwapigia simu akiwataka waandike barua za kujiuzulu lengo likiwa kuunda safu mpya ya uongozi kabla ya kuanza mchakato wa usajili.

Taarifa za awali zinasema kuwa baadhi walikuwa wamejiuzulu na wengine waligoma, lakini baadaye wote walikubali kujiuzulu akiwemo mwenyekiti wa bodi hiyo Salim Abdallah ‚Try Again‘.

Mbali yao hao wengine ni pamoja na Raphael Chageni, Hamza Johari, na Zulfikar Chandoo.

Kwa misimu mitatu, Simba imekuwa haifanyi vizuri kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, na msimu huu imeshindwa kabisa kupata nafasi ya kucheza Ligi ya Mabingwa Afrika, ambapo msimu ujao itashiriki Kombe la Shirikisho Afrika baada ya kumaliza Ligi Kuu ikishika nafasi ya tatu.

## Yanga yaahidi kushusha kina Pacome

INATOKA UK. 24

ambayo tayari wameshakata tiketi ya kushiriki baada ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

„msimu hyuu tumeishia robo fainali japo malengo yetu yalikuwa hatua ya makundi, msimu ujao tunataka kufika mbali zaidi, na kuw amiongoni mwa timu kubwa na tishio Afrika, hii ndio sababu tunafanya usajili wa maana na wenye tija,“ alisema Hersi.

Yanga pamoja na kutwaa Ubingwa wa Tanzania Bara mara ya tatu msimu huu, lakini imekuwa na kiwango bora na msimu wenye mafanikio, ambapo mbali na ubingwa huo, imetwaa Kombe la FA, pamoja na kufika robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika ikitolewa kwa mbinde na Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini kwenye hatua hiyo.

Michezo

Nip

Jumamosi Juni 8, 2024

Lu… unguka kuhamia Saudia



UKURASA 21




# Mo Dewji 'afyeka' wajumbe wake Simba

### ●●● Baadhi yao wafunguka, Barbara atajwa kuchukua nafasi ya...

**Faustine Feliciane na Adam Fungamwango**

WAKATI kukiwa na taarifa ya Mwekezaji wa Klabu ya Simba na Rais wa Heshima, Mohamed Dewji kuwaondoa wajumbe wote wa Bodi ya Wakurugenzi wa upande wake ndani ya klabu ya Simba, aliyekuwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Barbara Gonzalez anatajwa kurejeshwa na kukaimu nafasi ya Mwenyekiti wa bodi hiyo kwa muda.

Inaelezwa, Barbara atasimamia upatikanaji wa kocha mpya na kusaidiana na wateule wengine kufanya usajili wa maana ndani ya klabu hiyo kabla ya kurejea kwenye nafasi yake ya Ofisa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo.

Taarifa za uhakika kutoka ndani ya klabu hiyo zinasema uamuzi huo umefikiwa ili kuirejesha Simba kwenye makali yake ikikumbukwa chini ya Barbara ilikuwa ikifanya vizuri ndani na nje ya nchi huku kiongozi huyo akiwa na ushawishi mkubwa ndani na nje ya nchi.

Mmoja wa watu wa ndani ya klabu hiyo alikiri kutokea kwa mabadiliko hayo yenye lengo ya kuipa makali Simba msimu ujao.

„Ni kweli hilo limetokea, matokeo ya msimu huu ndio chanzo, imeonekana baadhi ya watu ndani ya uongozi hawawajibiki, tunakoelekea mwanga umeanza kuonekana ndani ya Simba, usajili utasimamiwa na watu makini na wenye uzoefu," alisema mtoa taarifa hiyo.

Alisema kila kitu kikiwa tayari wana simba watataarifiwa kufahamu nini kinaendelea na maamuzi yaliyochukuliwa.

„Simba ya msimu ujao itakuwa ya tofauti sana na msimu huu, heshima ya klabu itaanza kurudi na kuendelea kutamba kwenye soka la ndani na nje," alisema mtoa taarifa hiyo.

Katika hatua nyingine, mmoja wa wajumbe walioondolewa na Dewji, Rashid Shangazi alikiri kubwaga manyanga kwenye nafasi hiyo.

Shangazi, ambaye pia ni Mbunge wa Jimbo la Mlalo, amesema jana kuwa, amefanya maamuzi hayo kama sehemu ya uwajibikaji kwa ajili ya kutengeneza utawala bora, huku akiwasihi wenzake waliofanya kama yeye kuwapa ushirikiano watakaoteuliwa.

„Nimejiuzulu kama sehemu ya uwajibikaji, mwenendo wa timu haukuwa mzuri, wanachama wenzangu na mashabiki wana manung'uniko, miongoni mwa malalamiko yao ni kuona bodi na menejimenti tulishindwa kutekeleza wajibu wetu vizuri, wakati mwingine unawajibika kwa ajili ya kutengeneza utawala bora na wengine waje kusukuma gurudumu," alisema mjumbe huyo.

Hata hivyo alikanusha taarifa kuwa wameshinikizwa kujiuzulu, badala yake

INAENDELEA UK. 23

## Yanga yaahidi kushusha kina Pacome wengine

**Na Adam Fungamwango**

UONGOZI wa klabu ya Yanga umesema umepanga kusajili wachezaji wachache kuelekea msimu ujao, lakini wenye uwezo mkubwa kama waliopo au zaidi yao.

Rais wa Klabu hiyo, Injinia Hersi, amesema pamoja kuwa na kikosi kizuri, bora na imara, bado wataongeza baadhi ya wachezaji wachache, lakini wenye viwango vya hali ya juu kama waliopo au zaidi kwa ajili ya kukiongezea nguvu kikosi kuelekea kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu ujao.

Alisema kama kawaida yao, wapo makini katika suala ya usajili, hivyo kuwataka wanachama na mashabiki wa Yanga wasiwe na wasiwasi.

„Tumedhamiria kuwa na kikosi bora zaidi kitakachotikisa Afrika, kwa hiyo tutafanya usajili wa wachezaji watakaokuwa na faida ndani ya timu na kikubwa tunawekeza kwenye michuano ya Afrika, ili tufanye vyema huko tunalazimika kufanya usajili utakaoongeza nguvu ya kututoa hapa tulipo na kufikia kule tunapotarajia, tunataka kuwa na akina Pacome au Aziz Ki wengi ndani ya kikosi" alisema Hersi.

Mbali na hayo alisema kwa sasa wanaendelea kuwaongeza mikataba wachezaji ambao wanaona wanafaa kuendelea nao kwa matakwa ya benchi la ufundi, huku wale ambao wataonekana hawakidhi mahitaji ya klabu watawapisha wapya kuendelea pale walipoishia.

Alisema lengo la uongozi ni kuona timu hiyo inafanya vizuri zaidi kwenye mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >